**Zitto** atamba kumaliza zogo la ardhi Mbarali kwa dakika 10

UKURASA 2

**Usimamizi** ghala pembe za ndovu umulikwe, tukio moto lichunguzwe

UKURASA 4

**Wataalamu:** Haya ndiyo madhara ya kubandika kope

UKURASA 14



**Ferguson: Namisi sana kuinoa Man United**

UKURASA 22


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Septemba 22, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581807

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Polisi yaanika kiini cha mauaji

UKURASA 2



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Mwenza wake, Mama Mbonimpaye Mpango, wakiwasili katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, kushiriki kilele cha Kongamano la Nne la Uhuru wa Kidini la Afrika jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

## Makonda ageukia mitume feki, Mpango ataka tafakuri ya dini na siasa

UKURASA 7

MAKALA MAALUM

## Dawa wanaokojoa kitandani hizi hapa

• **Wenyewe** watoa ushuhuda wa madhila wanayopitia, wataalamu waanika undani wa tatizo.. *Endelea Ukurasa 3*

MICHEZO SIMBA KAZI MOJA TU LEO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kushoto), akizungumza na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Saudi Arabia, Mwanamfalme Abdul Aziz Bin Saudi Al- Saudi, nchini humo jana, kabla ya kutiliana saini hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya nchi hizo katika udhibiti wa matukio ya uhalifu kupitia Jeshi la Polisi na majanga mbalimbali kupitia Jeshi la Zimamoto. **PICHA: WMNN**

# Polisi yataja mambo matatu chanzo cha mauaji Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi limebaini chanzo cha mauaji yaliyotikisa Jiji la Dodoma, likieleza kuwa kuna shida kuu tatu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, amesema mauaji hayo yalisababishwa na kisasi, wivu wa mapenzi na imani za ushirikina.

Amesema kuwa katika ufuatiliaji wa jeshi hilo, tayari watu wanane wamekamatwa na wengine watatu wameshafikishwa mahakamani kwa mashtaka ya mauaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Kamanda Katabazi alisema kuwa kutokana na hali hiyo, moja ya mikakati waliyoweka ni kuhakikisha wanashirikiana na wananchi kuwakamata wahalifu kwa kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi.

"Jeshi la Polisi limejipanga kukabiliana na matukio ya uhalifu mkoani hapa, Wanahabari waendelee kuhabarisha kile kinachofanywa na jeshi. "Matukio haya yamekuwa mengi, lakini Jeshi la Polisi litahakikisha linakabiliana na wahalifu wa aina hii ili kutokomeza uhalifu unaojitokeza," alisema.

Kamanda huyo aliwaomba wananchi wasiogope kwenda kutoa taarifa polisi pale wanapoona kuna vitu hawavielewi katika mitaa mbalimbali wanamoishi na kusisitiza kwamba hakuna polisi atakayetoa siri za watoa taarifa.

Katika hatua nyingine, Kamanda Katabazi alisema wamekamata watu wawili wanaotuhumiwa kutengeneza noti bandia za Sh. 10,000 kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Alisema jumla ya Sh. 520,000 zimekamatwa pamoja na mashine ya kutengeneza fedha bandia, ambazo huzitumia kubambika watu au kununua bidhaa mbalimbali madukani.

Kamanda Katabasi aliwataka wafanyabiashara wawe makini pale wanapopokea fedha kutoka kwa wateja wanaokwenda katika maduka yao kupata huduma mbalimbali.

# Uboreshaji sekta ya afya wasogeza huduma za kibingwa kwa wananchi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imesema uboreshaji miundombinu na kuwapo vifaa tiba katika sekta ya afya umesaidia kuokoa maisha ya wanaotaka huduma za kibingwa kama upandikizaji figo na upasuaji wa moyo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliyasema hayo jana wakati akizindua Kituo cha Afya Makoga, wilayani Wanging'ombe, mkoani Njombe kilichojengwa kwa Sh. milioni 500.

Mkenda alisema kuwa awali watu walikuwa wanafariki dunia kutokana na kushindwa kwenda kutibiwa nchi za nje kwa kukosa fedha.

Alisema uboreshaji huduma, ukiwamo ufungaji vifaa umerahisisha upatikanaji wake maeneo mbalimbali nchini.

"Uwekezaji uliofanyika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) unasababisha hivi sasa hospitalini hapo kupokea wagonjwa kutoka nchi za Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Burundi kupata huduma za afya na hii ni juhudi za makusudi za Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Prof. Mkenda. Alisema kwa sasa mtu akipata tatizo la figo utaalamu wa kubadilisha na kuwekewa nyingine unapatikana nchini.

"Leo ukienda pale Dodoma, Hospitali ya Benjamin Mkapa tuna uwezo. Serikali imewekeza, unachukua figo ya mtu mwingine unapandikiziwa wewe na unapona na unakuwa imara kabisa.

"Nimeona mtu amefanyiwa upasuaji huo wa kuwekewa figo, mtu wa kwanza kabisa bado yupo hai mpaka leo hii," alisema Prof. Mkenda.

Prof. Mkenda alisema ujenzi wa Kituo cha Afya Makoga na kuwapo vifaa tiba vya kisasa, kutawasaidia wananchi kuacha kutembea umbali mrefu hadi mjini Njombe kufuata huduma za afya, zikiwamo za upasuaji.

"Kuletwa kwa vifaa na huduma hii katika kituo chenu inamaanisha ukiwa mjamzito unataka kufanyiwa upasuaji au dharura yoyote, huna haja ya kukimbilia mjini Njombe, huduma zote zitapatikana hapahapa," alisema.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Julius Peter, alisema yote yanayofanyika ni utekelezaji ilani; waliahidi Watanzania watasogeza huduma karibu na makazi yao.

Mbunge wa Wanging'ombe ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais - Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia afya, Festo Dugange, alisema miaka minne iliyopita wananchi hao walikuwa wanatibiwa katika zahanati ndogo licha ya kata hiyo kuwa na idadi kubwa ya watu.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zakaria Mwansasu, alisema serikali imepeleka vifaa vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 185 pamoja na Sh. bilioni sita kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya shule na afya.

Mganga Mfawidhi wa kituo hicho cha afya, Joseph Chota, alisema kilipokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto, maabara, upasuaji, jengo la kufulia, jengo la kuhifadhia maiti, nyumba ya mtumishi na kichomea taka.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Makoga, akiwamo Ruth Chaula, walisema kabla ya ujenzi wa kituo hicho, wajawazito walikuwa wanapata adha kubwa pindi wanapohitaj huduma ya upasuaji.

# Zitto atamba kutatua mgogoro wa ardhi Mbarali kwa dakika 10

**Na Halfani Chusi**

KIONGOZI mstaafu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe ametaja mbinu za kutatua mgogoro wa ardhi unaoendelea Mbarali, mkoani Mbeya.

Amesema mgogoro unaweza kutatuliwa kwa kung'oa nguzo za mipaka (bikoni) zilizowekwa katika makazi ya wananchi zinazowaonesha wamo katika eneo la hifadhi.

Zitto amesema kuwa kama angekuwa ameshika dola, angetumia dakika 10 tu kutatua mgogoro huo.

Akizungumza na wananchi wa Mbarali jana ikiwa ni mwendelezo wa ziara za viongozi wakubwa wa chama hicho waliojigawa kikanda, Zitto alisema:

"Kinachoitwa mgogoro wa ardhi uliko Mbarali ni kitu kidogo tu. Ni kuzitoa bikoni kutoka katika makazi ya wananchi na mashamba na kuzirudisha katika mpaka wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na mgogoro utakuwa umekwisha, njia ni ndogo kabisa."

Zitto alisema njia nyingine ni serikali kuunda tume ya kijaji kwa ajili ya kupitia mipaka yote iliyo karibu na hifadhi na kuchora upya ramani ya matumizi ya ardhi.

Akisimulia uzoefu wake katika migogoro ya Mbarali alipochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma ambayo jukumu lake lilikuwa kuchunguza kuhusu ubinafsishaji mashamba, Zitto alisema kazi yao ya kwanza walianzia Mbarali Estate na Kapunga.

"Moja ya mambo ambayo kila wakati ninayaeleza kwa wananchi, ni namna ambavyo Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilikuwa kimechoka na bado kimechoka, ni namna walivyoendesha mchakato wa ubinafsishaji.

"Tulipokwenda katika Kijiji cha Kapunga kukutana na wananchi, walitueleza kuwa mwaka 1984, serikali ilikwenda kwao kuwaomba ardhi kwa ajili ya mradi wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na kuipatia hekta 3,000 kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji.

"Ilipofika mwaka 1999, serikali ikashindwa kuendesha mradi ule, ikaamua kuubinafsisha, wakatangaza tangazo la kubinafsisha. Katika tangazo lile wakatangaza kwamba wanabinafsisha hekta 3,500.

"Wao walipewa hekta 3,000, hekta 500 ndio zilikuwa sehemu ya Kijiji cha Kapunga. Nilikwenda bungeni nikauliza serikali kwamba mmeamua kuwauza wanakijiji na mashamba yao?

"Bahati nzuri wakati ule Bunge lilikuwa Bunge kwelikweli. Nikapeleka ile ripoti bungeni, nikaeleza haya yote, wabunge wakabubujikwa machozi.

"Spika palepale (Samwel Sitta) Mwenyezi Mungu alaze roho yake mahali pema, akaagiza yafanyike marekebisho ya mkataba wa mauzo, wanakijiji warejeshewe ardhi yao. Ndivyo ambavyo tuliwaokoa wananchi wa Kapunga," alisema.

Zitto aliwasifu aliowaita "mashujaa wa Mbarali" kwa kufikisha malalamiko yao mahakamani kupingwa na kupokwa ardhi ambayo ni haki yao na kuahidi chama chake kitawapa tuzo.

Alisema hatua hiyo imesaidia mpaka leo wako katika eneo hilo kwa sababu serikali ilishindwa kuthibitisha kwamba maeneo yale ni maeneo ya hifadhi na wananchi walithibitisha ni maeneo yao.

"Hii ni nchi ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara. Tunaposema taifa la wote na maslahi ya wote, tunataka kila mtu aweze kuishi ndani ya nchi hii na kufaidi matunda ya nchi hii na siyo wachache waishi kama wanyama na kuuawa ovyo," alitamka Zitto kwa hisia kali.

Aliwaomba wananchi wa Mbarali kuchagua viongozi wanaotokana na chama cha ACT-Wazalendo, ili wawasaidie kutatua changamoto zao.

Msingi wa tatizo hilo umeelezwa kusababishwa na mchakato wa kuwahamisha wakulima na wafugaji katika kata tisa na jaribio la kutangazwa kufutwa vijiji vitano lililofanywa kuanzia mwaka 2022.

Ni mwendelezo wa utekelezaji Tangazo la Serikali (GN) Na. 28 la mwaka 2008, lilolenga kupanua eneo la Hifadhi ya Taifa Ruaha kwa kumega maeneo ya wananchi.

Hata hivyo, tangazo hilo lilipingwa vikali na wananchi, Zitto akiwaomba kuendelea kushirikiana kulinda haki yao.

MAKALA MAALUM

# Dawa wanaokojoa kitandani hizi hapa

Na Neema Emmanuel



KAMA una mtazamo hasi kiasi cha kumzodoa anayekojoa kitandani, basi unakosea! Wataalamu wa afya wamesema ni jambo la kawaida linalohitaji tiba ya kisaikolojia.

Wapo wanaokumbwa na changamoto hiyo kuanzia umri wa utoto hadi wanapoingia katika ndoa, na mara kadhaa imekuwa ikisambaratisha ndoa.

Daktari Steven Katwale kutoka Hospitali ya Rubya, wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza, anasema watoto wengi wanakumbana na changamoto ya kukojoa kitandani, hasa wakati wa usiku.

Anasema hali hiyo ni ya kawaida japo imekuwa inawashtua wazazi, akisisitiza kuwa ni muhimu kuelewa sababu zake na namna ya kukabiliana nazo.

Mtaalamu huyo anataja baadhi ya sababu ambazo zinachangia mtoto kukojoa kitandani ni pamoja na mabadiliko ya kisaikolojia na matatizo ya kiafya.

"Sababu nyingine zinaweza kuwa msongo wa mawazo. Watoto katika umri huu mara nyingi wanahitaji muda zaidi ili kujifunza kudhibiti mkojo wao, na ni muhimu kwa wazazi kuwa na uvumilivu na kuelewa kwamba hii ni hatua ya kawaida katika ukuaji," anasema.

Dk. Katwale anasema sababu nyingine zinazowagusa wanaokojoa kitandani hadi utu uzima, ni pamoja na unywaji pombe kupitiliza.

"Nyingine ni kunywa maji kupitiliza muda mfupi kabla ya kulala, matumizi ya baadhi ya dawa za kuondoa chumvi mwilini (diuretic drugs) na uwezo mdogo kibofu kuhifadhi mkojo - mara nyingi husababishwa na uvimbe katika kibofu," anafafanua.

Daktari huyo pia anasema kuziba kwa kibofu, maambukizi katika kibofu, pia kuwapo matatizo ya kiafya, mfano kisukari, shinikizo la damu na tezi dume kunaweza kusababisha mtu kuwa kikojozi.

"Kuna vyanzo vingi sana, hata kupata mimba za utotoni, malezi ya mtoto - kutokumwamsha kukojoa akiwa na umri mdogo, homoni hazijakaa sawa na maambukizi kwenye njia ya haja ndogo (U.T.I) ni tatizo pia," anasema.

Mtaalamu huyo anasema katika kuwasaidia watoto wenye hali hizo, wazazi wanaweza kuchukua hatua kama vile kuanzisha ratiba ya kwenda msalani kabla ya kulala, kuhamasisha unywaji maji wakati wa mchana na kuepuka vinywaji vyenye vileo usiku.

Pia anasema ni lazima wazazi au walezi wajifunze namna ya kuzungumza kwa upole na mtoto wao kuhusu hali hiyo ili kumsaidia kujiamini na kujifunza kudhibiti.

Vilevile, Dk. Katwale anashauri wenye changamoto hiyo waepuke kumeza dawa zinazosababisha kukojoa wakati wa usiku, badala yake wanywe mchana au saa sita kabla ya kulala, wapate muda wa kulala mchana angalau saa sita hadi nane.

Vilevile daktari huyo anasema ni lazima watu wabadili mfumo wa maisha, akitolea mfano kupunguza unywaji pombe kupindukia na kuwahi hospitalini kwa ajili ya kupima pale wanapoona tatizo limezidi.

**WAZAZI WALONGA**

Baadhi ya wazazi wenye watoto walio na changamoto hiyo, wanaeleza namna walivyoendelea na tatizo hilo hadi umri mkubwa, huku waathirika wakijichukia.

Stella Julian, mzazi wa watoto wawili, mkazi wa Jiji la Mwanza, anasema mtoto wake wa kiume alikuwa na changamoto ya kukojoa kitandani kwa muda mrefu.

"Nilifanya kila jitihada ikiwamo kumpa maji yaliyolowekwa katika sufuria ya ugali, maji ya mchele na dawa mbalimbali ambazo watu walikuwa wakiniambia, lakini sikufanikiwa.

"Mawazo yaliongezeka pale alipoingia kidato cha kwanza, alitakiwa kwenda shule ya bweni, aisee usiombe...!

"Nilinunua godoro nikalazimika kuvalisha mfuko wa plastiki. Nilipata mawazo sana, mwanangu pia alikuwa anajisikia vibaya sana. Alianza kujichukia lakini nilimpa moyo, sikumtenga!

"Nilifanya sana maombi, nilimwombea mwanangu, hakika Mungu alisikia kilio changu, aliacha tu mwenyewe kukojoa kitandani," anasema.

Elizabeth Kennedy, mkazi wa jijini Mwanza, ni mzazi wa watoto wanne; wote wana changamoto ya kukojoa kitandani, hasa wanapokunywa vimiminika vingi nyakati za usiku - maji, juisi, soda au chai.

"Mtoto anaweza kupitisha siku tatu hadi nne, anakojoa kitandani. Sijawahi kutumia dawa yoyote. Kuna ambaye ninayemfamu alikuwa anakojoa mpaka darasa la saba, alipofaulu kwenda kidato kwanza, wazazi walishindwa kumpeleka shule ya bweni kwa kuhofia kuchekwa na wanafunzi wenzake," anasema.

Jothamu Radiance, pia mkazi wa Mwanza, anasema mke wake amekuwa akimwamsha mtoto wao mara mbili au tatu usiku na asipofanya hivyo, hukuta amejikojolea.

"Tumejaribu kutafuta tiba hatujafanikiwa, japokuwa tunapata maelezo mengi, wengine wanasema ni ugonjwa wa kurithi, mapepo machafu na mambo mengi, bado hatujapata tiba mpaka sasa, yuko kidato cha nne.

"Kuna watu walitushauri tumbebeshe godoro apitiswe mitaani, niliona huo ni udhalilishaji, nilimkataza mama yake asifanye hivyo, imani yangu ninaona ipo siku ataacha mwenyewe," anasema Radiance.

**WASAIKOLOJIA TIBA**

Msaikolojia Tiba kutoka Somedics Polyclinic Health Centre, Saldin Kimangale, anasema tatizo la kukojoa kitandani kitaalamu wanaliita 'enuresis'.

"Ni tatizo la kibaiolojia na kisaikolojia, huwapata watoto na watu wazima ambapo mtu anashindwa kudhibiti haja ndogo wakati amelala.

"Linatambuliwa kwa watu wenye umri wa zaidi ya miaka sita. Husababisha aibu na wasiwasi. Sababu za kibaiolojia ni kama vile kuchoka au kuzeeka kwa mfumo wa mkojo na kurithi kwa njia za vinasaba.


"Kisaikolojia (vyanzo vya tatizo hili) ni pamoja na kuwapo msongo, wasiwasi... Ziko pia sababu za kimaumbile katika mfumo wa mkojo. Sababu za kimazingira ni pamoja na kunywa vimiminika nyakati za usiku," anasema.

Kimangale anasema athari zake ni pamoja na aibu, kujiona duni na hata kujitenga; kwa watu wazima aibu na hisia za kutokuwa na uwezo zinaweza kuwa kali zaidi.

"Kwa watoto, wazazi hukosa uvumilivu, hali inayoweza kuzidisha msongo wa mtoto na hasa wakiwachapa kama njia ya kukomesha tabia hiyo.

"Kwa watu wazima, kukojoa kitandani kunaathiri uhusiano wa kimapenzi au kijamii kutokana na aibu na kujihisi kutojiweza. Njia za kutibu ni pamoja na kufanya mazoezi ya kibofu, kuzuia kunywa vinywaji kabla ya kulala na matumizi ya 'alarms' (kengele za kuamsha)," anasema.

Mtaalamu huyo anaeleza zaidi kuwa zipo pia tiba kwa njia ya mazungumzo zinazofanywa na wanasaikolojia tiba ili kumsaidia mwenye tatizo hilo kuondokana nalo.






# Usimamizi ghala la pembe za ndovu umulikwe

**Na Mwandishi Wetu**

FEBRUARI 28, 2024, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliagiza Jeshi la Polisi kumkamata Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, anayetuhumiwa kushiriki uchepushaji fedha za umma zaidi ya Sh. milioni 213.

Akiwa ziarani wilayani Serengeti siku hiyo, Waziri Mkuu Majaliwa aliwataja wahusika wa uchepushaji huo, ambao alisema wanashirikiana na watumishi wengine watatu kutoka Kitengo cha Treasury Single Account (TSA) cha Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Majaliwa aliutaja ni mtandao wa hujuma dhidi ya fedha za umma ambao si tu umebainika wilayani Serengeti, bali pia uko katika maeneo mengine nchini, ikiwamo mkoani Kigoma ambako nako alishabaini shida hiyo katika ziara zake zilizotangulia.

Kwa mujibu wa Majaliwa, wahusika wa wizi huo wa fedha za umma, wanafikia hadi kusafirisha fedha hizo kwa mabasi, wakiweka mamilioni ya shilingi katika mabegi ya nguo.

Wakati umma ukisubiri kuona hatua zinazochukuliwa dhidi ya watumishi hao, wakiwamo hao wanaotoka ofisi nyeti - Ofisi ya Rais, baadhi wakiwa wameshafikishwa mahakamani na kufunguliwa kesi za uhujumu uchumi na utakatishaji fedha, kuna dosari nyingine katika usimamizi wa ghala la pembe za ndovu nchini.

Kulikoni? Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ameangazia suala hilo, akipendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia pembe za ndovu nchini.

CAG pia anapendekeza wizara iandae mfumo madhubuti wa taarifa zote zinazohusiana na pembe za ndovu, ukiwamo mpango mkakati wa taarifa za upotevu kutokana na matukio yasiyotarajiwa kama vile moto.

Shida ni nini? CAG anasema kuwa wakati wa ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Maliasili na Utalii, amebaini kuwa Mei 16, 2022, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, aliunda timu ya uhakiki wa mali ambayo ilijumuisha wajumbe kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA),

DW, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Anasema timu hiyo iliundwa kwa lengo la kuanzisha mchakato wa kuhesabu na kupima akiba ya nyara katika ghala la pembe za ndovu, jijini Dar es Salaam.



**CAG anasema kuwa wakati wa ukaguzi, ghala la kuhifadhia nyara hizo lilikuwa katika hali mbaya kutokana na kuwa na nafasi ndogo, paa kuvuja, hewa chafu, mazingira machafu, umeme usio imara, ukosefu wa kamera na vifaa vya kuzima moto.**

CAG anasema alibaini, pamoja na mengine, kutopatikana taarifa sahihi za pembe za ndovu zilizohifadhiwa kwa ajili ya kufanya tathmini na kuzipima upya pembe hizo.

Anasema pia alibaini hali isiyoridhisha ya pembe zote zilizohifadhiwa kiasi cha kusababisha kuharibika ubora na hadhi yake.

"Kwa maoni yangu, ukosefu wa udhibiti sahihi wa pembe za ndovu unaweza kusababisha upotevu wa taarifa zinazohusiana na pembe hizo,"

CAG alibaini shida nyingine ya kushindwa kuhuisha rejista juu ya hali na thamani ya pembe za ndovu, programu iliyotumika kurekodi na kusajili akiba ya pembe za ndovu na nyara zingine kutounganishwa na seva kuu ya programu ya wizara kwa sababu programu hiyo ilikuwa imepitwa na wakati.

CAG anasema katika ripoti yake kuwa, baadhi ya pembe za ndovu zilikosa taarifa zake za maandishi huku zingine zikiwa na taarifa zisizosomeka kutokana na ubovu wa paa la kuhifadhia, jambo linalosababisha kuvuja kwa paa hilo.

Anaongeza kuwa amebaini pia zana za kuwekea alama zilizotumiwa kurekodi taarifa kuhusu pembe za ndovu, ziliandikwa kwa wino unaoweza kufutika, hivyo kuzifanya ziweze kufutika kwa urahisi.

CAG anasema kuwa wakati wa ukaguzi, ghala la kuhifadhia nyara hizo lilikuwa katika hali mbaya kutokana na kuwa na nafasi ndogo, paa kuvuja, hewa chafu, mazingira machafu, umeme usio imara, ukosefu wa kamera na vifaa vya kuzima moto.

CAG anasema kuwa mbali na hayo, pia amebaini kuwa mwaka 2013, kulikuwa na tukio la moto katika ghala la pembe za ndovu ambalo lilisababisha kupotea kwa taarifa muhimu zinazohusiana na pembe za ndovu zilizohifadhiwa.

CAG anasema ni jambo la kushangaza kuwa hakuna uchunguzi uliofanyika ili kubaini chanzo cha moto huo na madhara yake hadi wakati wa ukaguzi wake.

"Kwa maoni yangu, ukosefu wa udhibiti sahihi wa pembe za ndovu unaweza kusababisha upotevu wa taarifa zinazohusiana na pembe hizo," anahadharisha.

CAG anasema taarifa kuhusu pembe za ndovu ni muhimu katika kesi za kisheria dhidi ya ujangili na juhudi zingine zinazolenga kudhibiti vitendo vya ujangili.

Vilevile, CAG anabainisha kuwa Menejimenti ya Wizara ya Maliasili na Utalii imethibitisha kuwapo upungufu huo huku ikiahidi kufanya uhakiki wa nyara kila baada ya miaka mitatu hadi minne, kulingana na upatikanaji wa rasilimali.

Kwa mtazamo wangu, haya yaliyobainishwa na CAG yanapaswa kufanyiwa kazi, ikizingatiwa nchi bado inakabiliwa na changamoto ya ujangili, hasa wa tembo na faru ambao kuna kipindi waliripotiwa kuwa hatarini kutoweka nchini.

Vilevile, hoja hiyo ya CAG inapaswa kufanyiwa kazi kikamilifu, ikizingatiwa Sekta ya Utalii ni tegemeo katika kuingiza fedha zote za kigeni nchini, ikiajiri watu 600,000 ofisini na wengine zaidi ya milioni mbili iliowapa ajira zisizo za moja kwa moja. Sekta hii pia iliingiza Sh. trilioni 8.575 nchini mwaka 2022/23.

Kwa msingi huo, ujangili ukifumbiwa macho, pia kuwapo udanganyifu katika ghala la kuhifadhi nyara hizo za serikali, kutahatarisha uhai wa wanyamapori wanaolengwa zaidi na majangili, hasa ndovu na faru, hivyo kuweka rehani uchumi wa nchi.

## Shule zaagizwa kupanda miti isiyopungua 100

Na Maulid Mmbaga

MKUU wa Wilaya ya Temeke, mkoni Dar es Salaam, Sixtus Mapunda, ameagiza shule zote za serikali kuhakikisha zinapanda miti isiyopungua 100, ikijumuisha ya matunda na kivuli, ili kuongeza chachu ya utunzaji mazingira.

Vilevile, amewataka wananchi kuachana na desturi ya kuweka sakafu kubwa katika maeneo yanayozunguka makazi yao, badala yake kupanda maua na miti itakayosaidia kufyonza maji nyakati za mvua na kuepusha mafuriko.

Mapunda aliagiza hayo jana wakati wa upandaji miti 200 katika Shule ya Msingi Madenge, wilayani Temeke.

"Wanafunzi wote wanapaswa kuona umuhimu wa utunzaji mazingira kwa kila mmoja kupewa mti wake aulee toka darasa la kwanza hadi saba. Tusisingizie maeneo, kuna watu majumbani wanaweka sakafu uwanja mzima haupumui, ardhi haipumui.

"Tukianza kwa mwanafunzi, akiwa na tabia ya kupanda miti kuanzia shuleni, ataipeleka hadi nyumbani, mimi ninaamini tukiamua kweli ndani ya miaka mitatu, Dar es Salaam itakuwa tofauti kwa kiwango cha juu, ukiwa Mbagala ukitoka kwenda Chamazi, unaweza kuona uko nchi nyingine," alisema Mapunda.

Mkuu wa Wilaya huyo alisisitiza wananchi kuacha tabia ya kupanda miti isiyokuwa na faida, badala yake wapande ya matunda pamoja na mboga ili wafaidike kwa chakula.

"Tubadilike tupande vitu vinavyotusaidia na tuache 'ushamba' wa kuweka sakafu kila mahali, hayo mambo yalishapitwa na wakati. Zamani yalikuwa na tija, lakini kwa sasa hayana faida kutokana na hali ya mabadiliko ya tabianchi," alisema Mapunda.

Pia alishauri kuwekwa miundombinu mizuri itakayosaidia maji yakiwamo ya mvua badala ya kusababisha mafuriko, yapate njia ya kupita.

Mapunda alisema serikali ina wajibu wa kutengeneza miundombinu, lakini kila mwananchi ana jukumu la kulinda mazingira yanayomzunguka.

# Dar yazalisha taka tani 4.5 kwa siku

Na Joseph Mwendapole

TAKWIMU zinaonesha kuwa licha ya Jiji la Dar es Salaam kuzalisha taka ngumu tani 4.5 kwa siku, ni asilimia 6.5 tu ya taka hizo zinazorejelezwa kuwa bidhaa mbalimbali.

Hayo yalibainishwa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzingatiaji na Utekelezaji Sheria katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Hamad Taimur, wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu uhifadhi wa mazingira.

Alisema Wilaya ya Temeke inaongoza kwa kuzalisha tani 1,494 za taka kwa siku, ikifuatwa na Ilala inayozalisha taka tani 1,320, Kinondoni tani 982, Ubungo tani 828 na Kigamboni tani 228.

Alitaja aina ya taka zinazorejelezwa kuwa ni plastiki, karatasi, vyuma chakavu, makopo ya aluminium, kioo na taka zinazooza.

Alisema kiasi cha taka oza zinazorejelezwa katika Jiji la Dar es Salaam ni tani 8.9 kwa mwezi ambapo tani 3,800 hurejelezwa katika kituo cha Bonyokwa, tani 3,200 Vingunguti, tani 1,500 katika kituo cha Mabwepande pamoja na vituo vingine.

Alisema serikali imekuwa inaandaa miongozi ya udhibiti wa taka ngumu kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imewezesha kujengwa vituo vya kuchakata na uchambuzi wa taka ngumu na inafanya mapitio ya Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Taka Ngumu za Mwaka 2024.

Alisema serikali imeendelea kujengea uwezo wa viongozi na wataalamu katika ngazi za wizara, mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuwawezesha kuboresha mifumo ya usimamizi wa taka ngumu.

Kuhusu changamoto, alisema kuna shida ya uelewa na mwitikio mdogo wa wananchi kuhusu namna ya kutenganisha taka katika ngazi ya kaya pamoja na uhaba wa miundombinu stahiki kuwezesha utenganishaji taka.

Alisema hali hiyo husababisha kuongezeka kwa wingi kwa taka zinazotupwa katika madampo licha ya kwamba zingeweza kurejelezwa na kuwa bidhaa zingine.

Alitaja changamoto nyingine ni uhaba wa miundombinu stahiki ya udhibiti wa taka ngumu ambazo ni pamoja na miundombinu ya kuhifadhi, kutenganisha, uondoshaji, usafirishaji na utupaji taka.

Alisema kumekuwa na uzingatiaji hafifu wa mipango miji inayosababisha kuwapo ujenzi wa makazi yasiyozingatia mipango husika na hivyo kuchangia kuwapo changamoto katika ukusanyaji taka zinazoweza kurejelezwa.

"Kumekuwa na mwamko hafifu wa matumizi ya mbolea itokanayo na taka na kusababisha mahitaji hafifu ya mbolea zitokanazo na taka zinazooza kwa jamii hususani kwa wakulima," alisema.

Ofisa huyo alisema serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha usimamizi wa taka ngumu na kukabiliwa na ongezeko kubwa la uzalishaji taka ngumu unaotokana na ongezeko la watu, shughuli za kiuchumi na ukuaji wa miji.

"Tukumbuke kuwa kila mmoja wetu ana jukumu kubwa la kulinda na kuyatunza mazingira kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya nchi yetu kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo, tusidhani mazingira ni jukumu la watu fulani," alisema.



Wananchi wakichagua vyombo katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Saudi Arabia kuipa mbinu za kisasa Polisi kudhibiti uhalifu

Na Romana Mallya

TANZANIA imetia saini hati ya makubaliano na Serikali ya Saudi Arabia inayogusa sekta mbili muhimu za usalama ya udhibiti wa uhalifu kwa kutumia utaalamu na teknolojia ya hali ya juu kwa Jeshi la Polisi.

Makubaliano hayo pia yanagusa udhibiti wa majanga mbalimbali, yakiwamo ya moto, ajali za barabarani na maporomoko kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Hati hiyo ya makubaliano kwa upande wa Tanzania imetiwa saini na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni na kwa upande wa Saudi Arabia, imetiwa saini na Mwanamfalme Abdul Aziz Bin Saudi Al- Saudi, huku pande zote mbili zikionesha nia ya kubadilishana uzoefu na vifaa mbalimbali vinavyotumia teknolojia katika udhibiti wa matukio ya uhalifu.

"Ninachukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani wa Saudi Arabia kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika ziara hii ambayo leo hii imepelekea kukamilisha utiaji saini kuhusu hati za makubaliano mbili.

"Tunakwenda kufungua milango ya kushirikiana kwa mapana zaidi katika maeneo hayo mawili. Itakwenda kufanya sasa nchi yetu kupitia Jeshi la Polisi kufaidika na fursa mbalimbali za ushirikiano, zikiwamo katika kujenga uwezo wa askari wetu katika maeneo mbalimbali na kubadilishana uzoefu na teknolojia ya jeshi letu," alisema.

Waziri Masauni alisema amefarijika kuona serikali ya Saudi Arabia imeweka msisitizo katika maeneo ambayo Tanzania imeweka nguvu kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kutoa huduma bora kwa wananchi," alisema Waziri Masauni.

Katika hafla hiyo, waziri huyo pia aligusia usalama wa kimtandao, akisisitiza kuwapo kipengele hicho katika hati ya makubaliano ili kudhibiti uhalifu wa mitandaoni ambao hivi sasa umeanza kushika kasi nchini.

"Tumeona wenzetu wameweza kuimarika sana katika matumizi ya teknolojia kudhibiti uhalifu wa kimtandao, hivyo ni imani yangu kwamba, kupitia ushirikiano ambao tumetia saini kwenye hati ya makubaliano, tunakwenda kufanikisha dhamira njema ya Rais Samia Suluhu Hassan kuimarisha Jeshi la Polisi katika eneo hilo.

"Kama mnakumbuka serikali imewekeza fedha nyingi kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 100 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa mbali na vifaa vingine ambavyo tayari vishaingia nchini mwaka huu ambavyo vinahitaji askari wetu wawe na uwezo na weledi wa kuvitumia, sambamba na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambao tayari walishaanza kupokea magari," alisema Masauni.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Saudi Arabia, Mwanamfalme Saudi Al- Saudi, alisema wako tayari kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kudhibiti matukio ya uhalifu.

Waziri huyo pia alieleza namna Saudi Arabia ilivyodhibiti matukio mbalimbali ya uhalifu, akisema kuwa kila mwaka maelfu ya waumini wa dini ya Kiislamu na wageni kutoka mataifa mbalimbali hufika nchini humo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabaraza ya ardhi yasiwe chanzo cha migogoro

**MIGOGORO** ya ardhi katika maeneo mengi nchini imekuwa chanzo cha vurugu kwa wakulima na wafugaji.

Suala la wakulima na wafugaji kugombea ardhi limekuwa likishamiri katika maeneo mbalimbali nchini huku wakulima wakitaka ardhi ya kulima na wafugaji wakitaka sehemu ya kulishia mifugo yao.

Hali hiyo imesababisha baadhi yao kuingia katika mapigano na hata kusababisha vifo na wengine kubaki na vilema vya kudumu.

Migogoro hii inaweza kutatuliwa kama kukiwa na mipango mizuri kutoka kwa watekelezaji ambao ni mabaraza ya ardhi.

Hata hivyo, kumekuwapo na malalamiko kuwa baadhi ya viongozi wa mabaraza hayo ndio chanzo cha migogoro hiyo huku wakituhumiwa kuhusishwa na suala la rushwa.

Hivi karibuni kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, amekemea kile alichodai "rushwa kwa baadhi ya viongozi katika mabaraza ya ardhi".

Akitoa mfano wa Wilaya ya Kiteto alipokuwa katika mwendelezo wa ziara zinazofanywa na viongozi wakuu wa chama hicho kuwa ni

ni moja ya 'makao makuu ya migogoro ya ardhi' ambayo inasababishwa na mgongano kati ya wakulima na wafugaji.

Anaigeukia serikali kwa kutoonesha kwamba migogoro itakwisha kwa kujipanga vizuri na kuongeza kasi kushughulikia matatizo hayo.

Kimsingi kinachotakiwa ni kuwapo kwa mifumo bora ya kutatua changamoto za ardhi na wanaoongoza mabaraza ya ardhi kuwa na elimu ya kutosha ya namna ya kuitatua.

Wananchi wamekuwa wakiingia migogoro ya wenyewe kwa wenyewe kwa kuuziwa ardhi mara mbili mbili kutokana na baadhi ya watendaji kutokuwa na weledi na kuweka mbele maslahi yao binafsi.

Hata hivyo Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akiwa mkoani Kilimanjaro, alionya watendaji wa ardhi wanaokiuka maadili.

Katika mkutano wake na wananchi, Naibu waziri huyo, amewaonya watendaji hao kutokubali kuwa hawafai kuwa kwenye nafasi zao.

"Nikimwambia Katibu Mkuu huyu utendaji kazi wake unaripotiwa kwamba hafai, tutatuma vyombo vitakuja kukutafakari upya.

"Usikubali dawati lako liwe chanzo cha mgogoro, upelekwe kwa Mkuu wa wilaya, kwa Mkurugenzi, kwa mbunge na jambo lile uliloanzisha wewe linakwenda mpaka kwa Rais. Haiwezekani! Kila mtu ajitafakari."

Upatikanaji wa hatimiliki za ardhi pia umekuwa tatizo kubwa kiasi cha kusababisha wananchi wanaponunua ardhi kuamua kuiendeleza bila kusubiri taratibu.

Ukiritimba na ucheleweshaji kwa sababu tu baadhi ya maofisa kutaka rushwa limekuwa tatizo kubwa.


Naibu Waziri huyo pia alitoa maelekezo kwa Ofisi za Wasajili wa Hati nchini kuharakisha mchakato wa utoaji hatimiliki za ardhi ili wananchi waweze kunufaika nazo ikiwa ni pamoja na kuaminiwa kupata mikopo katika taasisi za kifedha.

Ameliagiza dawati la usajili lisilaze kazi kwa kutoa hati ili ziende kwa wananchi.

Kadhalika maofisa ardhi wanaojihusisha na ugawaji kiwanja kimoja mara mbili wameonywa na kwamba wizara yake itachukua hatua kali za kinidhamu dhidi ya mtumishi yeyote atakayekiuka maadili ya utumishi wa umma kwa taaluma yake.

Kwa mujibu wa Naibu waziri, Ofisa yeyote atakayehusishwa kwenye jambo la kugawa kiwanja kimoja mara mbili, atachukuliwa hatua kali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuepuke nadharia na imani ya dini na afya, tukiumwa twende hospitalini

Na Sabato Kasika

**KATIKA** kuimarisha afya, serikali inajenga zahanati kila kijiji, vituo vya afya kila kata, hospitali za wilaya, mikoa na za rufani za kanda ili kutoa huduma kwa wananchi.

Ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa mwaka 2008 unaoelekeza kuwa na vituo hivyo vya kutolea huduma katika ngazi husika - kijiji hadi kitaifa.

Hata hivyo, jukumu hilo si la serikali tu, bali hata taasisi za kidini nazo zina hospitali zake, lengo likiwa ni kusaidiana na serikali kutoa huduma za afya kwa waumini wake na kwa Watanzania kwa ujumla.

Hatua hiyo inaonesha kuwa pamoja na kuwapo kwa huduma za kiroho, waumini wanahitaji kupata huduma za afya pale wanapougua, hivyo ni wazi kuna mipaka kati ya nadharia ya imani na huduma ya afya.

Maana yake ni kwamba, muumini anapougua, anakwenda hospitalini kupimwa kisha kupatiwa matibabu. Hawezi kwenda kanisani au msikitini kwa kuamini kuwa Mungu atamwezesha kupona.

Kama ingekuwa ni hivyo, kusingekuwa na haja ya taasisi za dini kujenga zahanati, vituo vya afya au hospitali kwani kuna mipaka kati ya nadharia ya imani na afya na ndio maana taasisi hizo zinatoa huduma za afya.

Isivyo bahati, kuna dhana imejengeka miongoni mwa waumini wa madhehebu mbalimbali ya dini ambao wamefikia kutokwenda hospitalini pale wanapoumwa, wakiamini wameokoka, hivyo inatosha. Kwa mazingira haya, watu wanaweza kuumia, hivyo ni vyema wakatafakari kwa kina na kuchukua hatua sahihi, wakitambua kuwa kuna haja kuweka mipaka kati ya nadharia ya imani na dini na suala la afya.

Hata kama mtu ameokoka, anapoumwa ni vyema akaenda hospitalini kutibiwa na kama watazunguka katika hospitali mbalimbali bila kupona, ndipo wamwachie Mungu afanye kazi.

Si vizuri mtu kuhatarisha maisha yake kwa ugonjwa ambao anajua wazi kuwa unatibiwa hospitalini, lakini anakataa kwenda kwa sababu ya kuwa na msimamo wa kuzingatia dhana ya imani.

Yawezekana mtu akawa ameambukizwa Virusi vya Ukimwi (VVU), akawa ameanza kutumia dozi ya kupunguza makali ya virusi hivyo, halafu akakatisha kwa sababu tu ameokoka. Kitendo hicho ni sawa na kujiangamiza mwenyewe.

Ninaamini kuokoka kupo, lakini kusichanganywe na masuala la tiba. Mtu anapoumwa, aende hospitalini kufanyiwa vipimo ijulikane anaumwa nini badala ya kukimbilia katika nyumba za ibada.

Jamii itambue mipaka kati ya nadharia za imani na umuhimu kutibiwa pale muumini anapougua ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza iwapo mgonjwa atazidiwa.

Suala na mtu kuwa na imani yake ya dini liko palepale, lakini lisimfanye akakiuka utaratibu wa matibabu kwa kuwa dawa zina sehemu yake na Mungu naye ana sehemu yake katika maisha ya mwanadamu.

Tuangalie Sheria ya UKIMWI iliyopitishwa na Bunge mwaka 2008, inaelekeza mambo mbalimbali muhimu yanayohusu mtu aliyeambukizwa VVU na jinsi anavyotakiwa kufanya.

Sheria hiyo ni mahususi ili kuzuia maambukizo ya VVU, kuendeleza na kutunza afya ya jamii, na inatoa mwongozo wa huduma inayotakiwa kwa watu walioambukizwa au kwa wale walio katika hatari ya kupata maambukizo.

Inataja haki za mtu anayeishi na VVU kuwa ni kupata huduma za afya ya mwili na akili, kwa kadri ya ubora unaohitajika, kupata matibabu sahihi ya magonjwa nyemelezi na kupata haki zote alizonazo binadamu mwingine yeyote ambaye hajaambukizwa virusi.

Sheria hiyo pia inataja wajibu wa mtu anayeishi na VVU, kuwa ni kulinda wengine wasipate maambukizo ya ugonjwa na kushiriki na kuchangia katika maendeleo ya kisayansi na mafanikio yake.

Wizara ya Afya inatakiwa kuhakikisha ARV pamoja na huduma nyingine muhimu za afya na dawa vinapatikana, na kwamba mtu yeyote haruhusiwi kumbagua au kumnyanyasa mwenye VVU.

Ni wazi kwamba kila mmoja akizingatia jinsi sheria hiyo inavyotaka, hakutakuwa na njia ya mkato ya kukabiliana na VVU, badala yake, aliyembukizwa atatumia ARV kwa ajili ya kupunguza makali ya virusi hivyo.

# Makonda ageukia manabii, mitume feki

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda amesema Tanzania hivi sasa inao viongozi wengi wa dini, lakini si maarufu kwa neno la Mungu au uponyaji kama walivyofanya mitume.

Kutokana na ombwe hilo, kwake yeye kama Makonda, Mwana wa Mungu, anawatangaza ni maaskofu feki, wachungaji feki, manabii feki na mitume feki.

Akitoa salaam za serikali jana katika viwanja vya Kisongo, jijini Arusha wakati wa mkutano wa injili wa Mtume Boniface Mwamposa (Buldoza), Makonda alisema:

"Wana wa Mungu niwaambieni, ukimwona kiongozi wa dini mwenye jina lakini umaarufu wake hautokani na kazi ya mikono ya Kristo, hautokani na kazi za Mungu; jua huyo ni kiongozi wa dini feki.

"Nchi yetu sasa hivi ina viongozi wengi wa dini lakini si maarufu kwa neno la Mungu. Maarufu kweli si kwa kazi ya uponyaji kama wanavyofanya mitume. Hao mimi Makonda, Mwana wa Mungu, ninawatangaza ni maaskofu feki, ni wachungaji feki, ni manabii feki, ni mitume feki.

"Yaani hii kofia ya ukuu wa mkoa, kuna wakati mimi huwaza, ninasema 'eeh Mungu wangu eeh...! Sijui ningechomoka kidogo ningekaa huku nihangaike na neno? Na watu ni waoga!

"Eti mimi leo hii, ukuu wa mkoa, kanipa Samia (Rais Samia Suluhu Hassan), eti kutwa ninamsifia Mbowe (Freeman-Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo -CHADEMA), si nitafukuzwa kazi jamani?" alihoji Makonda.

Katika mkutano huo wa Mwamposa, Makonda, alisema amepewa atoe salamu na salamu zenyewe ndizo hizo.

Makonda aliwaeleza mamia ya waumini waliojitokeza katika mkutano huo kwamba watu wasiseme ameenda kusema kwa Mwamposa kwa kuwa "yeye ana kifua".

"Ninaweza kuchanganya makamasi na machozi, ninapiga magoti kumlilia Mungu kwa sababu ya Tanzania.

"Mimi ni zao la maombi na wala sioni aibu. Apostle (Nabii) ananifahamu nikiwa chuoni, na wengi walitegemea nitakuwa mchungaji. Nikasema aah, wengine tumeitwa tu, lakini tunampenda Mungu. Kwani nyie (ninyi) watu wa Arusha si mnamwona Mungu? Kwani kuna manyanyaso? Fanya kazi ya aliyekuita, nawe utabarikiwa," Makonda alisema.



Fundi wa kampuni ya ujenzi ya Sinohydro, akiendelea na ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka (BRT), katika barabara ya Bibi Titi Mohamed, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA:JUMANNE JUMA**

# Mpango ataka tafakuri dini na siasa

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ametaka kufanyike tafakuri kuhusu baadhi ya viongozi wa dini au madhehebu kujiambatanisha na chama cha siasa na kupeleka maoni yao binafsi ya kisiasa na kutafsiriwa kuwa ndiyo maoni ya dini au madhehebu wanayoongoza.

Amesema hali hiyo inachangia changamoto kubwa katika uhusiano na ushirikiano baina ya serikali ambayo haina dini na baadhi ya viongozi wa dini wenye mrengo dhahiri wa kisiasa.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana wakati wa Kilele cha Kongamano la Nne la Uhuru wa Kidini Barani Afrika lililofanyika katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Alitoa wito kwa watumishi wa Mungu kutafakari mwenendo unaozidi kuota mizizi wa ugomvi na vurugu za aina mbalimbali miongoni mwa waumini wa imani moja, wakiwamo baadhi ya viongozi wa dini.

Dk. Mpango alisema kuwa hivi sasa kunashuhudiwa viongozi wakiondoana au kufukuzana katika nyumba za ibada kwa sababu mbalimbali, yakiwamo matumizi mabaya ya fedha na mali za kanisa, kugombea madaraka, ajira za upendeleo, rushwa na kukosekana haki katika uchaguzi.

"Viongozi wa dini wanayo nafasi na heshima ya pekee katika jamii Tanzania na nchi nyingine za Afrika, kama wawakilishi wa Mungu hapa duniani, hivyo ni jambo la muhimu kudhibiti tamaa ya mali iliyopitiliza na uchu wa madaraka na kurudi katika wito halisi," alisema.

Dk. Mpango aliwasisitiza kurudi katika utaratibu wa kusemana na kuonyana kwa upendo kanisani na misikitini badala ya kufanya hivyo mitandaoni.

Pia aliwasihi viongozi wa dini kuhimiza umuhimu wa kuishi katika hali ya usalama na amani na mazingira kama njia mojawapo ya kudumisha uhuru kwa kidini.

Aliwataka wafanye hivyo kwa kuwa mazingira na rasilimali zake kama vile maji ni muhimu katika kumwabudu Mungu na kuwezesha binadamu, wanyama, mimea, ndege na wadudu kuishi pamoja kwa amani na kwa kutegemeana.

Dk. Mpango alisisitiza kuhakikisha wanakuwapo walimu wa dini katika muda unaotolewa mashuleni ili kutunza na kurithisha maadili mema kwa vizazi vya sasa na vijavyo na kukemea maovu kwa nguvu zote.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye amani na utulivu katika Bara la Afrika ambapo kiini cha hali hiyo ni misingi iliyowekwa na waasisi wa taifa iliyosisitiza umoja, mshikamano, kuheshimiana na kuondoa tofauti za kidini, kisiasa, rangi au kabila.

"Uhuru wa kidini nchini unatambuliwa na kulindwa na Katiba na serikali inashirikiana kwa karibu na viongozi wa dini zote hasa katika sekta za afya na elimu na kushauriana kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza na kuhakikisha shughuli za dini zinaendeshwa kwa amani na utulivu," alisema.

Mwenyekiti wa Kanisa la Waadventista Wasabato, Unioni ya Kaskazini mwa Tanzania, Mch. Mark Malekana, alisema malengo ya kongamano hilo ni kuhimiza amani, heshima ya binadamu, haki za binadamu na uhuru wa dhamira miongoni mwa Waafrika.

"Pamoja na tofauti zilizoko za itikadi, imani, utamaduni na rangi ni muhimu kutambua jambo muhimu la kutuunganisha na sisi sote ni binadamu," alisema.

Kongamano la Nne la Uhuru wa Kidini la Afrika lilianza Septemba 17 mwaka huu, likihusisha mataifa yote ya Bara la Afrika na kuhudhuriwa na wanasheria, majaji, wanadiplomasia, viongozi waandamizi serikalini, wasomi kutoka taasisi mbalimbali za Afrika, wawakilishi wa mahakama, wawakilishi wa Umoja wa Afrika (AU) na viongozi wa dini mbalimbali.

## DC: Viongozi wa dini wahamisishe ushiriki Uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, ameowaomba viongozi wa dini kutumia nafasi zao kuelimisha na kuwahamisha wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na kuhubiri maadili mema.

Machali alitoa rai hiyo juzi wakati wa kikao na viongozi wa dini ambacho kilikuwa na lengo la kujadili masuala yanayohusu mmomonyoko wa maadili, uzalendo, amani pamoja na ushiriki wa viongozi hao katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

"Ningependa kutumia nafasi hii kuwaomba mkawaeleze waumini kuhusu kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakofanyika Novemba 27 mwaka huu.

"Tujitokeze kwa wingi katika kampeni, tujiandikishe kwenye daftari la orodha ya wapigakura na siku ya uchaguzi tuchague viongozi wetu kwa amani," alisema.

Machali aliwakumbusha viongozi hao wa dini kuhusu mchakato wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, akiwaomba kutumia nafasi zao kuwaeleza wananchi ifikapo Septemba 25 mwaka huu, wajitokeze kuboresha taarifa zao kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Akizungumzia maadili, kiongozi huyo wa wilaya alisema viongozi wa dini wana jukumu kubwa katika kuhubiri amani na kulinda maadili ya jamii.

"Twendeni tukahubiri amani na upendo kwa waumini wetu, nitashangaa siku nikisikia watu wa Mkalama wanagombana kwa sababu ya dini, kila mmoja aheshimu imani ya mwenzake," alisema.

Mch. Manase Msengi kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Nduguti, akizungumza kwa niaba ya viongozi wenzake, alimshukuru na kumpongeza Mkuu wa Wilaya ya Mkalama kwa kukutana na viongozi wa dini kwa ajili ya kujadili masuala ya maadili, uzalendo na amani hasa katika kipindi hiki cha mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuwataka wananchi wajitokeze kushiriki uchaguzi huo.

# MATUKIO KATIKA PICHA




Mitambo ikinyanyua nguzo kwa ajili ya kufunga taa za kuongozea vyombo vya moto, katika barabara ya Kawawa, eneo la Ilala Boma, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Mkuu wa Mahusiano ya Vyombo vya Habari wa Vodacom Tanzania, Annette Kanora (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam hivi karibuni, kuhusu kampeni ya Twende Butiama yenye lengo la kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kupanda miti, huduma za afya na elimu. Kulia ni Meneja Uhusiano na Chapa wa benki ya Stanbic Tanzania, Annette Nkini. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Naibu Kamishna wa Polisi, Mwamini Rwantale, akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uchunguzi wa Kisayansi Duniani, katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda (wapili kushoto), Ofisa Misitu Temeke, Neema Daudi (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Bima ya Afya ya Jubilee, Dk. Harold Adamson (wa pili kulia), wakipanda miti katika Shule ya Msingi Madenge, Dar es Salaam juzi, kwa kushirikiana na taasisi ya Aga Khan, ikiwa ni mwendelezo wa programu yao ya utunzaji mazingira. Jumla ya miti 200 ya matunda na vivuli, ilipandwa shuleni hapo. **PICHA: MAULID MMBAGA**



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, Moses Machali akizungumza na viongozi wa dini wakati wa kikao chenye lengo la kujadili masuala yanayohusu mmomonyoko wa maadili, uzalendo, amani pamoja na ushiriki wa viongozi hao katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, wilayani humo, jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

MAISHA

SEPTEMBA 22, 2024

Nipashe


Baba, Mama na Mwana

Jumapili



Ukurasa 14

ROSTI YA KABEJI






# UVAAJI WA 'MLEGEZO' TABU TUPU

Ukurasa 13

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| O | | J | E | M | B | E |
| N | | | | K | | N |
| G | | F | A | O | | D |
| O | V | U | | S | I | E |
| Z | | M | O | I | | L |
| W | | B | | | | E |
| A | M | A | N | A | | A |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


ARA, DAU, MBU, TIN, OTANA, FUNDA, NINDU, TAMKA, AMBULIA, MAKALIO

## AMSHA AKILI

JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 4 | 2 | 3 | |
| 1 | | 2 | 4 |
| | | | |


## TOA TOFAUTI 5



# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanangu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuaambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mashambulizi ya binti kwenye ndoa!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Ninaamini kabisa yapo mambo mengi unajifunza kupitia safu hii kuhusu maisha ya kila siku ndani ya familia zetu.

Wiki iliyopita nilizungumzia misingi ya malezi ya mabinti zetu. Nikakazia kwamba kinamama wengi wamepumbazwa kuwadekeza mabinti zao wawapo nyumbani na kazi zote kufanywa na dada wa kazi.

Kwa kufanya hivyo na kwa kutokujua, kumbe wanawaandaa kinadada hao kuwa kinamama bora wa baadaye. Matokeo yake, mabinti zao wanakwenda kuwa vituko wanapoolewa. Ndio maana ndoa nyingi zinakufa mapema kutokana na msingi mbovu wa malezi.

Wiki iliyopita nilisema kuzaa ni tofauti na malezi, na matunzo ni tofauti na kulea. Kulea ni kuongoza, kulea ni kuelekeza, ni kumwandaa mtoto wako. Na aliyepewa jukumu la kulea ni mwanamke. Mwanamume halei, bali anatoa matunzo.

Hebu leo niendelee kuwatolea macho mabinti zetu. Mama ndiye awezaye kuweka msingi wa maisha ya binti yake. Ndiye anayetoa mwelekeo wa maisha ya binti awe mama wa aina gani baadaye.

Tabia njema au mbaya ya mama, asipokuwa makini, ndiyo atakayokuwa nayo binti yake. Kanuni hii ipo wazi katika moja ya maandiko ya Mungu pale ilipoandikwa; "Tazama, kila mtu atumiaye mithali hii kinyume chako, akisema, kama mama ya mtu alivyo, ndivyo alivyo binti yake." (Ezekieli 16:44).

Njia atakayochagua binti au kijana, ndiyo hatma ya maisha yake. Njia ni mwelekeo utakaochagua wewe binti uwe mama gani wa baadaye. Na mwelekeo huo usiende peke yako, mtafute Mungu akuongoze.

Ndiyo maana neno la Mungu linasema, "Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe". Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atanyoosha mapito yako (Mithali 3:5-6).

Mungu alimpa mwanamke nguvu ya ufinyanzi ndani ya tumbo lake. Ni mama anayetengeneza kizazi kilichobarikiwa. Wanawake ni hatma ya uzao wao.

Mabinti wengi wanaolewa wakidhani kuwa ndoa ni mteremko hakuna vita. Ukiwa nje ya ndoa ni shwari. Ukishaingia ndani, ndipo unakutana na vituko vyote. Wale waoga ambao hawakupewa misingi ya ndoa/malezi, ni wepesi kukata tamaa.

Kwa wale waliofundishwa vema jinsi ya kuhimili misukosuko ya ndoa, ndio wanaotetea ndoa zao. Unapoingia katika ndoa, binti hukutana na wakwe, mawifi, mashemeji ndugu upande wa mume. Hawa nao humulika ndoa hiyo, humfuatilia binti kuona je, ni sahihi katika boma lao?

Yapo mambo mbalimbali binti huyu atakutana nayo katika safari yake hiyo ya ndoa. Kama wazazi wake walimlea vyema, yapo mashambulizi hayatamgusa.

Lakini ikiwa malezi yake yalikuwa ya kudekezwa, hakufundwa mambo ambayo aweza kukutana nayo na jinsi ya kuyakabili, furaha ya ndoa yaweza kuwa shubiri.

Wapo mabinti wanaoingia kwenye ndoa na kukutana na familia ya wacha Mungu, wengine wachawi/washirikina, wenye maagano na waabudumiungu, walevi, wagomvi, waongo, wenye hasira kali na kadhalika.

Tabia hizi zote mtu hawezi kuzijua hadi achangamane nao. Na hii ni kwa pande zote upande wa kijana na pia upande wa binti.

Na tabia hizi ukishaingia katika ndoa hujitokeza taratibu. Inawezekana tayari ndoa imeshadumu miaka miwili hadi mitano ndipo tabia zinajitokeza.

Unaingia katika ndoa binti kumbe kupika hujui, kwanini mama mkwe au mawifi wasikuseme, wasikushangae? Binti amepambana, amezaa watoto wake wawili na mume akajenga nyumba nzuri na gari lao.

> "Ndiyo maana neno la Mungu linasema, "Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe". Katika njia zako zote mkiri yeye, naye atanyoosha mapito yako (Mithali 3:5-6).

Mawifi na mama mkwe wanawatembelea toka kijijini wanakuta maendeleo hayo. Wanaanza kuona wivu na kumchokonoa mkamwana. Eti haiwezekani ajengewe nyumba nzuri vile wakati kijijini nyumba ya udongo. Tayari vita katika ndoa.

Lazima binti awe na uvumilivu kwani vita katika ndoa haikosekani. Usiondoke ukampa adui ushindi. Jiulize, mbona walikubali ndoa lakini hawakubali mafanikio?

Binti yampasa kujiandaa kuwa mama bora. Ni muhimu pia atambue kwamba yeye ni pumzi na mume wake. Yeye ndiye anayepaswa kusimama kujijenga nyumba yake.

Mwanamke mwenye hekima huijenga nyumba yake, lakini mpumbavu huibomoa kwa mikono yake mwenyewe. Isitoshe, mwenye mwenendo mnyofu humcha Mwenyezi Mungu, lakini mpotovu humdharau Mungu. Na mwenye kuwaka hasira haraka hutenda kipumbavu, lakini mwenye busara ana uvumilivu.

***Je, una maoni/kisa? Ujumbe 0715268581.Namba hii pia ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Samia amewashinda Mahulukutabu waliovuruga Ngorongoro

RAIS Samia Suluhu Hassan amewashinda kwa mbinu wale wachokonozi na wachochezi wa mambo, wanaoitwa kwa lugha ya Kizanzibar "mahulukutabu".

Septemba 17 mwaka huu, akiwa katika Shule ya Polisi Tanzania alikokwenda kuzungumza na makamishna, maofisa waandamizi wa polisi, makamanda na vikosi wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo, Rais alionesha kuchukizwa na mahulukutabu.

Kwa mujibu wa Rais Samia, mahulukutabu ni watu wenye hulka ya kutaka kuishi katika tabu tu wakati wote; utulivu na raha kwao si mahali sahihi.

Kwamba mahulukutabu yeye nchi ikiwa imetulia haoni raha, lazima atie mikikimiki.

Ninakubaliana na kauli ya Rais Samia, si kwenye R4 peke yake ndiko ambako kuna mahulukutabu.

Falsafa ya Rais Samia ya 4R, yaani Reconciliation (maridhiano au upatanisho), Resilence (ustahimilivu), Reforms (Mageuzi au Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga Upya), ndiyo inayomfanya ang'are na kuwaumiza vichwa mahulukutabu.

Mahulikutabu wako hata kwenye shughuli za uhifadhi, ambako dunia inaijua vilivyo Tanzania kutokana na utajiri ilionao wa vivutio vya utalii kama Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Tangu kuanza zoezi la kuhama kwa hiari wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro, Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha Juni 2022 hadi sasa, kumekuwa na kelele nyingi za wanaoitwa mahulukutabu.

Wanapiga kelele na kuwahadaa wananchi wa Ngorongoro, lakini hawaoni dhamira ya serikali kuwajengea makazi ya kudumu, kuwapa maeneo ya kilimo na ranchi ya malisho ya mifugo yao huko Kijiji cha Msomera, Kata ya Misima, Wilaya ya Handeni, Tanga.

Hata kule Saunyi, Kitwai na Meatu ambako wananchi hao wamehamia kwa hiari, mahulukutabu hawaoni kazi nzuri inayofanywa na serikali.

Hawasikii, hawaoni na wala hawana furaha kuona kazi kubwa inayofanywa na serikali kutangaza utalii wa Tanzania na kufanya Ngorongoro kuwa kitovu cha utalii wa Tanzania.

Hadi kufikia mwezi Agosti mwaka huu, kaya 1,598 zenye watu 9,618 na mifugo 39,779 zilikuwa imeshahama kwa hiari ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kupisha shughuli za uhifadhi ili kurejesha ikolojia yake baada ya makazi ya watu na mifugo kutishia uhai wa hifadhi hiyo.

Rais Samia kashasema tunapotaka kutekeleza falsafa ya R4, si kwamba tumetupilia mbali sheria zetu za nchi au tumeruhusu utovu wa nidhamu utokee ndani ya nchi yetu, la hasha!

Ameruhusu mbali na huduma zilizokuwa zimefutwa kisheria, takwa la kikatiba kwa wakazi wa Ngorongoro, mkoani Arusha na maeneo mengine nchini, kushiriki upigaji kura kwenye maeneo ya kiutawala ya vijiji 12,333 vilivyokuwa vimefutwa.

Hatua ya urejeshaji vijiji hivyo inatokana na maeneo yaliyokuwa yamefutwa awali kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 673 na 674.

Maeneo hayo yalihusisha pia Tarafa ya Ngorongoro inayokaliwa na idadi kubwa ya wafugaji wa jamii ya Kimasai.

Lengo la kuchukua hatua hiyo ni kuhakikisha maeneo hayo yanapata uwakilishi mzuri wa kiutawala pamoja na huduma za kijamii na kiuchumi zinazowiana na mahitaji ya wananchi wake.

Uamuzi wake, uzalendo wake na mapenzi yake kwa raia wake, vinafanya serikali kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya kisheria na utawala bora.

Na kwa muktadha huo, tayari serikali anayoongoza imetoa amri na notisi ya mgawanyo wa maeneo ya kiutawala katika serikali za mitaa.

Hata wananchi wa Ngorongoro wanakiri wazi kupitia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Marekani Bayo, kwamba wamepokea tangazo hilo kwa furaha.

Kwa nini? Ni kwa sababu vijiji 65 na vitongoji 242 wilayani humo, wananchi watashiriki katika uchaguzi na kupiga kura.

Mahulukutabu punguzeni hiyo kasi, tukajenge nchi yetu, amani yetu idumu na tukawe mfano nchi zote za Afrika na dunia.

Kongole Rais Samia kwa kuutangaza utalii wetu, tunakuunga mkono.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***







Ni siku ya kukumbukwa kwa Christopher Mahilane na mkewe Joyce John, baada ya kufunga ndoa yao takatifu Septemba 14 mwaka huu. Sherehe ilifanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga: **PICHA: SHABAN NJIA.**







# MITINDO

Na Moshi Lusonzo




## Uvaaji wa 'mlegezo' tabu tupu

Ukuaji wa mitindo ya mavazi ni suala pana na lenye kupita hatua mbalimbali ndani ya jamii kwa lengo la kutimiza matakwa na mahitaji ya wakati huo.

Katika kipindi hicho cha mpito kunaibuka aina mbalimbali za mitindo ya nguo na uvaaji na kuiacha jamii husika kuichakata na hatimaye kuikubali kama vazi rasmi.

Katika safari hiyo ndefu, vijana hasa wa kiume wanakuwa waathirika kutokana na kuwa watumiaji wakubwa.

Katika miaka ya karibuni kumezuka mtindo wa uvaaji wa nguo ambao unashusha chini sehemu ya kiuno na makalio ikionekana.

Si kwamba watumiaji wa nguo hizo wanaacha ikiwa wazi, la hasha, bali wanashusha suruali zao chini na kuacha eneo la makalio ikisitiriwa na nguo ya ndani au fulana. Wenyewe wanasema mlegezo.

Vijana wa kiume wanaopenda aina hiyo ya uvaaji ni wasanii wa muziki, filamu na hata mitaani tunapoishi.

CHANZO

Wataalam wanasema chanzo cha vijana kuathirika na mabadiliko ya mitindo ya mavazi inatokana na tabia zao za kujaribu, kujiamini na kujiona wanakwenda na wakati.

Kwa ujumla, kundi hili linataka kuona wanakuwa watu wa kwanza kuingia katika mabadiliko na ndio maana kila mara wanajikuta wakilaumiwa.

CHIMBUKO

Uvaaji wa nguo kwa mtindo wa mlegezo ulianza kutumika miaka ya nyuma nchini Marekani, ambapo ulihusishwa na watu wa mapenzi ya jinsia moja.

Toka kuasisiwa kwake umekuwa ukipigwa vita duniani kote, lakini kutokana na vijana kutumia kwa kiasi kikubwa imekuwa vigumu kutokomeza.

Hata hivyo, katika misingi ya kistaarabu uvaaji huo hauna staha na ndio maana serikali na watu binafsi wanapiga kelele.

UREMBO

Na Mary Geofrey





# Madhara kubandika kope

UREMBO wa kisasa katika nchi zinazoendelea ni sehemu ya mchango wa urembo na mvuto tunaouona kwa baadhi ya wanawake, kwa hakika unaleta hamasa kuangalia.

Hata hivyo, urembo huu huja na hatari zake ambazo wengi wanaweza kuzichukulia poa kwa kuwa hazitokei kwa haraka ama katika muda unaoweza kutolewa ushahidi.

Moja kati ya urembo unaofanywa na wanawake wengi wa kisasa ni kuweka kope za bandia juu ya kope halisi zinaleta mvuto hasa kwa wanaume.

Lakini hatari inayotokana na urembo huo ni kubwa zaidi ya matokeo ya muda mfupi.

Wataalam wanaeleza kuwa kope za bandia ambazo hugundishwa kwa kutumia gundi ya nywele inayotumika kugundisha nywele bandia kwa wenye vipara inaweza kuwa chanzo cha upofu kwa mtumiaji.

Gundi hiyo hupukutika taratibu sana kiasi cha kutoshtukiwa na kuelekea kwenye mboni ya jicho ambayo ndio moyo wa 'kuona'.

Endapo mtumiaji ataendelea kwa muda mrefu kutumia kope hizi bandia anaweza kujikuta anakuwa na tatizo la kuona ama hata upofu wa haraka katika maisha yake ya baadae.

Hata hivyo, hatari kubwa imeelekezwa kwa maduka ama vibanda vinavyotumia vifaa vya bei nafuu ikiwamo gundi inayotumika.

Ukwepaji wa gharama ama kutokuwa na uwezo wa kutumia gharama kubwa kuna mwingiza mrembo kwenye hatari zaidi.

Kuwa mwangalifu, urembo usiwe chanzo cha kuhatarisha afya yako. Kumbuka Afya ni uhai wa mwili wako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya fenesi

FENESI ni miongoni mwa matunda matamu yanayovutia wengi kuanzia kwenye ladha hadi rangi yake ya ndani.

Fenesi siyo tu linafaa kuliwa, bali linaweza kutumiwa kutengeneza juisi nzuri na ambayo utaipenda.

Juisi hii pia inafaida nyingi ambazo huupa mwili virutubisho muhimu ikiwemo Vitamini na madini chuma jambo linalofanya kutumiwa na watu wa rika zote.

Mahitaji

Mafenesi bakuli moja, parachichi nusu kikombe, maji, pasheni nusu kikombe, hiliki kijiko kimoja na sukari saizi unayopendelea.

Maandalizi

Hatua ya kwanza utayaosha matunda na kuanza kuyaandaa vizuri huku ukitoa zile tunda zinazopatikana katika fenesi, kisha utachukua blenda yako na kuikagua kama ni safi kwaajili ya matumizi.

Anza kuweka fenesi, passion (karakara), parachichi, hiliki, sukari na maji kwa pamoja katika blenda na kuanza kuvisaga kwa muda wa dakika sita hadi viwe laini na kuchanganyika vizuri.



Tumia blenda kwa muda wa dakika sita, ukipumzisha kila baada ya dakika moja ili kuepusha blenda kupata moto sana na kuharibika.

Utaendelea na hatua hiyo hadi utakapomaliza mchanganyiko huo wa matunda na viungo vyako.

Baada ya kumaliza kusaga utachuja hiyo juisi, kisha utahifadhi katika chombo kisafi na kama utapendelea utaweza weka katika friji (jokofu) lako ili iwe ya baridi au unaweza kunywa angali ipo hivyo hivyo.

Unaweza kunywa juisi yako kwa chakula chochote ukipendacho au hata pekee bila ya chochote.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya






# Hivi ndivyo unapaswa kusafisha sofa

KATIKA safu hii leo tunaangalia umaridadi katika usafi wa sofa, hili nalo ni kiungo muhimu cha kung`arisha na kuleta mvuto ndani ya nyumba.

Ni eneo ambalo katika usafi wa mambo mengine katika nyumba, linahitaji usafi, tena kwa umaridadi wa hali ya juu hususani kwa nyumba zenye familia kubwa.

Sofa zikifutwa kawaida au kwa kutumia maji, matokeo yake huwa si nzuri kwa kuwa badala ya kung`ara huanza kuchafuka na kuchakaa zaidi.

Kwa wale wanaomiliki sofa za vitambaa, wanatakiwa kutumia njia sahihi zaidi kusafisha badala ya kufuta kienyeji ili kuzitunza zisiharibike kwa sababu kitambaa ndicho kiko katika hatari zaidi ya kuharibika endapo utaratibu mzuri hautafuatwa wakati wa kusafisha.

Yapo maji maalum au kwa lugha nyingine 'spray' inayotumika kusafishia sofa hizo, ni vyema ukaitafuta hiyo kwa sababu inapatikana kwa wingi madukani.

Lakini kabla ya kuanza kutumia, hakikisha sofa zako zimepanguswa na kutolewa vumbi lililokuwa imeng`ang`ania kwa kutumia kifaa maalum cha kupuliza vumbi ama kwa kutumia kitambaa kisafi.

Baada ya kuhakikisha umesafisha kila kona, ndipo unatakiwa kuanza kuipulizia.

Kwa kuzingatia ujazo katika chupa hizo maalum za maji ya kusafishia sofa, unaweza kutambua utumie chupa ngapi na kwa sofa ngapi kulingana na ukubwa wa tatizo japokuwa ninaamini moja inaweza kutosha labda kama imechafuka kupitiliza.

Unachopaswa kufanya ni kupulizia katika sehemu ndogo ili wakati huo huo uwe unafuta na kitambaa kisafi na unatakiwa kufanya hivyo mpaka umalize.

Baada ya kumaliza kazi hiyo katika maeneo yote, unaweza kuliacha likauke na hapo ndipo utaanza kuona matokeo mazuri kwa sababu mng`ao wa rangi yake utakuwa mzuri zaidi. Kumbuka kwamba kufanya usafi huo katika sofa lako hakuhitaji gharama kubwa, endapo utafanya mwenyewe, isipokuwa uamue kutumia gharama kubwa kwa matakwa yako kwa kutumia wataalamu wa kukodi.

Pia, kadri utakavyojenga utaratibu wa kupenda kusafisha sofa lako mara kwa mara ndivyo gharama itazidi kuwa ndogo kwa sababu hutatumia spray nyingi kama ambavyo utasafisha zikiwa zimechafuka sana.

## Unaweza kutumia vyombo vya mbao pekee

Na Restuta James

WIKI mbili zilizopita, msomaji wangu kutoka Musoma alinitumia meseji kutaka kujua ubunifu wa matumizi ya mbao umeweza kutatua vifaa vyote vya jikoni.

Alinipa changamoto ya kupekua mtandaoni na maeneo yanayouza kazi za sanaa ili kujiridhisha kama kazi za wasanii wa kuchonga zimeongeza ubunifu, kutoka kwenye miiko, vibao vya kukunia nazi na vinu, hadi kutengeneza vifaa vyote vya jikoni.

Katika eneo wanakouza vifaa vya uchongaji Kariakoo, ubunifu umeleta masinia, bakuli, glasi, vijiko vikubwa na vidogo, visu vya kulia chakula, vikopo vya kuwekea chumvi, sukari na viungo mezani, pamoja na vifaa vya siku zote vnu, miiko na kibao cha kukuzia nazi.

"Sasa hivi unaweza kuamua nyumba yako ukatumia vifaa vya mbao kasoro tu sufuria na vingine vichache sana kama visu vya kukatia na chujio la kuopolea maandazi kwenye mafuta," anaeleza Mariamu Athanas, anayeuza aina hiyo ya vyombo.


Anafafanua: "Kwa wapenzi wa mbao, hakuna ambacho hawawezi kuchonga hapa nchini. Hata kama hakipo sokoni, ukienda na picha kwa wachongaji, unakipata kama kilivyo."

Hata hivyo, muuzaji wa vyombo vya udongo katika soko la Kariakoo, Khadija Ramadhan, anasema kwa wasiopenda vyombo vya mbao, wanaweza kujipatia vyombo vya rangi wazipendazo kwa kuwa vipo vya maumbo na rangi tofauti.

"Ukitaka rangi yoyote ya chombo, unaipata kama unavyoona kwenye nguo na rangi za nyumba. Kile unachotaka kikufurahishe ukiwa jikoni au kwenye meza ya chakula kwenye vyombo kipo," anasema.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
EEBABA! NISITIRI MJA WAKO SIOGOPI KIPIGO ILA NAOGOPA KICHEKO CHA UTOPOLO
WATOTO WA GADDAFI WA LIBYA
JUKWAANI
WE USITAKE KUNITIBUA KWA MASWALI YAKO NTAKUCHOKA!
MIE NAULIZA KUTEMBEA KWA MIGUU HADI KWA NKAPA HUKU NIME-BEBA BENDERA HATUTAONEKANA 'TUNAANDAMANA?'
SIJUI LEO CHAMA LANGU LITATOBOA?
CHAMA LAKO HALIJANISAIDIA KULIPIA CHUMBA USINIKWAZE
MBONA UNANIKATA MAINI?
UKITAKA KUBETI JITOSE TU, USITAKE NIKUHAKIKISHIE ALAFU BAADAE UNIJIE NA PANGA!
MGANGA 'JAU'
LEO BHANA MNATANDIKWA VIZURI TU.
'SUMBAWANGA' WAMEONESHA 'VIDOLE HIVI' EBU NITAFSIRIE
ULE MPANGO WETU WA KUANDAMANA SI UPO PALEPALE?
KILANGA' CHA KWENDA KUJAZA FRIJI 'MONCHWALI' SIKITAKI...

HABARI KIMATAIFA

# Mahakama nchini Kenya yaamuru Meta kushtakiwa

**NAIROBI,** KENYA

MAHAKAMA ya Kenya imeamuru kwamba kampuni mama ya Facebook Meta inaweza kushtakiwa katika taifa hilo la Afrika Mashariki kutokana na kufukuzwa kazi kwa wakaguzi wa maudhui na makandarasi.

Ilielezwa kuwa mahakama nchini humo ilitoa uamuzi huo jana, na kwamba mwaka jana wakaguzi wa maudhui walishtaki Meta na makandarasi wawili wa ndani, wakisema walipoteza kazi zao na Sama, kampuni ya Kenya yenye kandarasi ya kukagua maudhui ya Facebook, kwa kuandaa muungano.

Walisema waliwekwa kwenye orodha ya waliopigwa marufuku baada ya kutuma maombi ya kutafuta kazi yenye majukumu sawa katika kampuni nyingine, Majorel, baada ya Facebook kubadilisha makandarasi.

Mazungumzo ya kupata suluhu nje ya mahakama hayakuzaa matunda mwezi Oktoba mwaka jana.

Uamuzi wa Ijumaa wa Mahakama ya Rufaa uliidhinisha uamuzi wa awali wa mahakama ya wafanyakazi wa Kenya Aprili 2023 kwamba Meta inaweza kukabiliwa na kesi kuhusu kufutwa kazi kwa wakaguzi wa maudhui, ambayo Meta ilikata rufaa.

Pia ilikubali uamuzi tofauti mnamo Februari 2023 kwamba Meta inaweza kushtakiwa nchini Kenya kwa madai ya mazingira duni ya kazi, ambayo Meta pia ilikata rufaa.

"Hitimisho la matokeo yetu hapo juu ni kwamba rufaa za Meta, hazina mashiko na rufaa zote mbili zimetupiliwa mbali na gharama kulipwa kwa walalamikiwa," majaji watatu wa Mahakama ya Rufani walisema katika uamuzi wao siku ya Ijumaa. **TRT**




Kansela Olaf Scholz akizungumza na wakazi wa Brandenburg wakati wa ziara yake katika jimbo hilo la mashariki mwa Ujerumani **PICHA: MTANDAO**

# Scholz: Hatutaipatia Ukraine makombora ya Taurus

**BRANDENBURG,** UJERUMANI

KANSELA wa Ujerumani Olaf Scholz amesisitiza msimamo wake kwamba hatoipatia Ukraine makombora ya masafa marefu katika jaribio lake la kuwashawishi wapiga kura katika jimbo la Brandenburg.

Ilielezwa jana kuwa kiongozi huyo amekuwa akifanya kampeni kwa ajili ya chama chake cha Social Democratic (SDP) kabla ya uchaguzi unaotarajiwa kufanyika leo katika jimbo la Brandenburg.

Pia ilielezwa kuwa katiko eneo hilo la mashariki mwa Ujerumani chama chake kinapambana na chama cha mrengo mkali wa kulia Alternative fur Deutschland (AfD).

Aliwahakikishia wapiga kura kwamba Ujerumani haitoipa Ukraine makombora aina ya Taurus, licha ya Kyiv kuwahimiza washirika wake wa Magharibi kuipa silaha zaidi ili kukabiliana na wanajeshi wa Russia katika uwanja wa vita.

"Ingawa wengi wamejaribu kunirai, sitatoa makombora ya masafa marefu ambayo yana uwezo wa kufika hadi Moscow, nawahakikishia hili na nitasimamia msimamo huu," Scholz alisema.

Jimbo la Brandenburg linaongozwa na Dietmar Woidke wa chama cha SPD, japo chama hicho kinakabiliwa na upinzani wa AfD kuelekea uchaguzi wa siku ya leo.

Katika hatua nyingine, ilielezwa kuwa Ukraine imekuwa ikipambana na wanajeshi wa Russia kwa zaidi ya miaka miwili na nusu.

Licha ya kuungwa mkono na mataifa ya Magharibi, vita hivyo vimeenea hadi ndani ya Russia baada ya vikosi vya Ukraine kuliteka eneo la Kursk katika hatua ambayo huenda ikamshurutisha Rais Vladimir Putin kwenye meza ya mazungumo.

Scholz anatumai kuwa chama cha SPD kitashinda uchaguzi huo, akitaja ukuaji wa uchumi ulioshuhudiwa jimboni humo katika miaka ya hivi karibuni kama moja ya sababu ya kukuamini chama hicho.

"Kwangu mimi, ni muhimu sana kwa Brandenburg kuendelea kupiga hatua za maendeleo katika siku zijazo," Kansela huyo alisema wakati wa ziara ya awali aliyoifanya katika maonyesho ya filamu kwenye mji mkuu wa jimbo hilo, Potsdam karibu na Berlin. **DW**

## Israel yapinga kukamatwa kwa Netanyahu ICC

**JERUSALEM,** ISRAEL

KWA mara ya kwanza Israel imesema kuwa imepinga rasmi uamuzi uliotangazwa mwezi Mei mwaka huu na mwendesha mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) wa kuomba hati za kukamatwa kwa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, na Waziri wake wa Ulinzi, Yoav Gallant.

Israel inahoji mamlaka ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu katika kesi hii pamoja na uhalali wa ombi la mwendesha mashtaka.

"Nchi ya Israel leo 'jana' imewasilisha hatua yake kupinga rasmi ombi la mwendesha mashitaka wa ICC la kutaka kukamatwa kwa Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu na Waziri wa Ulinzi Yoav Gallant," ilisema.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Israel, Oren Marmorsstein, katika ujumbe wake kwenye mtandao wa kijamii wa X, alisema Israel inatilia shaka mamlaka ya ICC katika kesi hiyo pamoja na uhalali wa ombi la mwendesha mashtaka.

Mwendesha mashtaka wa ICC Karim Khan mwezi Mei aliomba hati za kukamatwa kimataifa kwa Benjamin Netanyahu na Yoav Gallant pamoja na viongozi kadhaa wa kundi la Hamas kwa madai ya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya ubinadamu katika Ukanda wa Gaza na Israel.

Alisema dhidi ya uamuzi huu, Israel iliwasilisha maoni mawili kamili ya kisheria, bila kutaja hati hizo zilitumwa kwa nani au mamlaka gani.

Kwenye hati ya kwanza, Israel ilibainisha kuwa suala hili lote ni wazi liko ndani ya mamlaka ya ICC, kulingana na msemaji huyo.

Kwenye hati ya pili, Marmorstein alibainisha kuwa Israeli inaeleza ukiukwaji wa mwendesha mashitaka wa sheria za Mahakama na kanuni ya kukamilishana, kwa kuwa hakuipa Israel fursa ya kutumia haki yake ya kuchunguza yenywe kuhusu shutma hizo zilizotolewa na mwendesha mashitaka kabla hajapeleka ombi lake Mahakamani.

**RFI**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Uke wenza fahari kwa wanaume, wanawake kwao majanga matupu



Na Adam Fungamwango

"KWELI mama Fatu nilipokuona, sikuamini macho yangu. Nilikuwa kama niko ndotoni mama Fatu shoga yangu. Ama kweli hujafa hujaumbika, naamini ya walimwengu, jinsi umbo lako lilivyobadilika ni masikitiko kwangu. Hebu nieleze umepatwa na maswahibu gani?"

Ni swali alilokutana nalo mama Fatu mara baada ya kukutana na shoga yake njiani. Aliulizwa swali hilo kwa jinsi alivyobadilika. Amefujika, amesawajika, amekonda. Unene wote umeisha. Shepu yote imeondoka.

Maneno haya yapo kwenye wimbo uuitwao 'Uke Wenza' uliotungwa na mwamamuziki Marijani Rajab mwanzoni mwa miaka ya 1980 akiwa na bendi ya Dar Intenational.

Mtunzi na mwimbaji huyo alikuwa akielezea juu ya kinachowapata baadhi ya wanawake wanaokwenda kuolewa na wanaume ambao tayari wana wake.

Ingawa si wote wanaopata shida, lakini ndani ya jamii kumekuwa na shida kubwa na watu wengi wameshuhudia kadhia na madhara ya uke wenza.

Inakuwa ni vita, patashika nguo kuchanika, wanawake kugombana wenyewe kwa wenyewe. Ukiona hadi wanamuziki wa dansi wameliweka kwenye hadhira jambo hili, ujue wameliona na si mara moja wala mara mbili.

Hata sisi wenyewe nadhani tutakuwa tumeshuhudia japo hata tukio moja la majirani au watu wanaotuhusu, au kuwafahamu juu ya jambo hili la uke wenza.

Hebu turudi kule njiani mama Fatu alipokutana na shoga yake, alijibu nini?

"Ooo ukwewenza, kweli uke wenza una mambo, ama kweli nimeona vituiko, unitizame nilivyokonda, sababu ya ukwenza.

Ukwewenza mimi sitaki jama sitaki, tena nimekoma hata kulisikia jina hilo sipendi. Ukewenza ni fahari kwa wanaume kwetu ni tabn. Hata mwanangu Fatu akiposwa na mwenye mke sikubali. Ukiolewa bora ukute mke mwezio mwenye imani. Kama si hivyo nakwambia ndugu yangu utajuta, hebu nitizame mwenzio mambo yaliyonifika. Hakuna sababu ila ni sababu ya ukewenza. Ukwewenza mimi hapana."

Hili ndiyo lilikuwa jibu la mama Fatu. Baadhi ya wanamuziki wa bendi ya Dar International ambao waliipigia bendi hiyo, wamesema kwenye mashairi hayo ambayo mama Fatu anajibu yalirekebishwa kwenye studio za Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

> **"Ndugu yangu Ete pole kwa yaliyokufika, Ete ulipoolewa, ulimkuta mwenzako nyumbani, pendo lako kwa mume wako, lilisababisha mwenzio, kuachika bure. Nyumbani alipoondika alikuendea kinyume yakakufika maradhi.**

Kamati ya kupitia maudhui kilimshauri Marijani kubadilisha baadhi ya mashairi kwani yake ya mwanzo yalikuwa makali sana na yanayochoma moyo kiasi kwamba hata wasikilizaji, hasa akinamama wangeweza kuangua vilio au kutoka na machozi.

Wanamuziki hao walisema Marijali aliendа mbali sana kwenye maneno ya mama Fatu aliyokuwa akimjibu shoga yake, kiasi kwamba aliingiza hata mambo ya ushirikina ambayo yalitolewa na kuwekwa hayo ambayo yameandikwa na kusikika kwenye wimbo huo.

Mama alikuwa akilalamika kufanyiwa mambo ya kishirikina na mke mwenzake kiasi kwamba kila anakokwenda kuangalizia kwa wataalam hawaoni ugonjwa, na wakiona wanamwambia ni mke mwenzake.

Bado mama Fatu anaendelea kulalama na kutoa ushuhuda kwa yaliyomfika kutokana na kukaa ukwewenza.

"Ukewenza mama, bora usikie hivyo hivyo. Ukewenza kweli hatari we mama, akinababa wanatuletea janga, fahari yao kwetu sisi matatizo."

Hayo ni kwa yaliyomfika mama Fatu. Kuna wimbo mwingine ambao ulitungwa na Juwata Jazz unaitwa 'Ete' ambao nayo unamhusu mwanamke aliyekwenda kuolewa matala, lakini yaliyomkuta, ni ya kusikitisha.

Dada yake alikwenda kumpa pole na akaelezea tukio zima kama lilivyoimbwa na Msondo Ngoma.

"Ndugu yangu Ete pole kwa yaliyokufika, Ete ulipoolewa, ulimkuta mwenzako nyumbani, pendo lako kwa mume wako, lilisababisha mwenzio, kuachika bure. Nyumbani alipoondika alikuendea kinyume yakakufika maradhi.

Mapenzi ya wake wawili, hayawezi kuwa ya kweli, yangelikuwa ya kweli Ete, yasingekufika. Tutajitahidi nduguzo maradhi yakutoke, Mola atakusaidia ndiye mwenye uwezo. Ungeyajua mama mapema, katu usingejitosa, ukewenza umekuponza Ete wateseka."

Ina maana hapa mke mkubwa alipoondoka akenda 'kufanya yake' na Ete akaugua maradhi yasiyojulikana. Haya yapo na yanatokea kwenye jamii. Mada hii inawahusu sana akinamama. Ningependa wale wote ambao wameshawahi kupatwa na mikasa hii, kuoina jirani au kwa ndugu zao, au hata kuhadithiwa na wenzao wanitumie ujumbe kwenye namba hiyo ya chini na tutazichapisha wiki ijayo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Uanzishaji Idara ya Ustawi wa Jamii inayojitegemea waiva

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesema iko katika hatua za mwisho kuanzisha Idara ya Ustawi wa Jamii inayojitegemea chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, ili kurahisisha na kuimarisha uratibu, usimamizi na utekelezaji afua za ustawi wa jamii nchini.

Taarifa za kuundwa idara hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Dorothy Gwajima wakati akifunga mkutano wa tatu wa mwaka wa maofisa ustawi wa jamii uliofanyika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Waziri Dorothy alisema lengo la kuanzisha Idara ya Ustawi wa Jamii itakayojitegemea ni kukidhi ongezeko la uhitaji wa huduma za ustawi wa jamii kisekta kunakohitaji taasisi madhubuti katika kusimamia na kuratibu utoaji huduma hizo katika jamii kupitia taasisi za umma, binafsi na wananchi kwa ujumla.

Kwa mujibu wa waziri huyo, hatua hiyo ni matokeo ya kukubaliwa kwa wasilisho la mapendekezo ya Haki Jinai kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Pamoja na mambo mengine, waziri huyo alisema mpango huo hivi sasa unasubiri maelekezo ya muundo wa idara hiyo kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

"Ninamshukuru sana Rais Samia ambaye ni Ofisa Ustawi wa Jamii namba moja kwa kutambua mchango wa kazi zenu na kuipa kipaumbele tasnia hata kubariki tuendelee kufanya mkutano huu kila mwaka, ili kupata nafasi ya kujifunza mambo mazuri kutoka kwa wenzetu.

"Tunapata nfasi ya kujadili namna ya kutatua changamoto za ukatili wa aina mbalimbali zinazokumba jamii yetu kwa sasa pamoja na namna ya kuboresha mazingira ya kazi tunapotekeleza majukumu yetu," alisema.

Waziri Dorothy alisema elimu itakayotolewa na maofisa hao itasaidia jamii kuelewa mambo mbalimbali ya huduma za ustawi, hasa huduma za unasihi kwa watoto, wazazi/walezi, huduma za uchangamshi wa awali ya watoto wadogo na huduma ya afya ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa makundi yenye uhitaji.

Alisema familia ndio taasisi pekee ambayo ni nguzo muhimu katika malezi bora inayomwandaa mtoto kuwa mwanamume au mwanamke bora wa baadaye, na familia ndiyo mahali salama kwa watoto kukua na kufikia utimilifu wao.

"Familia zimekuwa zinakumbwa na changamoto nyingi, zikiwamo umaskini, migogoro ya ndoa na familia, malezi duni kwa watoto inayopelekea kukosekana muunganiko na uhusiano hafifu kati ya wazazi au walezi na watoto wao, ambapo athari zake ni pamoja na watoto kukosa upendo wa wazazi au walezi.

> **"Ninamshukuru sana Rais Samia ambaye ni Ofisa Ustawi wa Jamii namba moja kwa kutambua mchango wa kazi zenu na kuipa kipaumbele tasnia hata kubariki tuendelee kufanya mkutano huu kila mwaka, ili kupata nafasi ya kujifunza mambo mazuri kutoka kwa wenzetu.**

"Kuendelea kuwapo mila na desturi za kukaa kimya na kuficha taarifa za vitendo vya ukatili hasa vinavyotokea ndani ya familia, kumesababisha kuendelea kuwapo vitendo vya ukatili na kukosekana huduma kwa waathirika, hali inayosababisha mmomonyoko wa maadili na tabia hatarishi kwa watoto," alisema.

Mwenyetiki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatma Tawfiq, alisema anatambua wataalamu hao wamefanya tathmini ya mambo yote yanayotakiwa ili kuboresha utendaji kazi na kutatua changamoto zao.

Alisema kamati yake itaendelea kushauri serikali kuongeza bajeti ili kuwawezesha maofisa ustawi wa jamii kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha.


Mkutano huo wa tatu wa mwaka wa maofisa ustawi wa jamii uliofanyika kwa siku tatu kuanzia Septemba 18 mwaka huu, ulibeba kaulimbiu ya "Tanzania Bila Ukatili Inawezekana, Imarisha Uhusiano Ndani ya Familia."

# HADITHI

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanaume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

# Nyuma ya Pazia-1

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




ILIKUWA kama kipanga au mwewe anavyonyakua kifaranga cha kuku. Mtu mmoja mrefu mwenye misuli aliyevaa fulana yenye mikono mifupi na jinzi lililopauka alimkamata ghafla na kumnyanyua mtoto mmoja wa kiume na kukimbia naye kwenye gari. Ilikuwa ni kazi rahisi sana kwa mtu huyo kama kumsukuma mlevi kwenye utelezi.

Sauti ya kitoto iliyokuwa ikilia, “mama aaa, mama aaa, sitaki, niachie...” Ndiyo zilizowashtua watu waliokuwa pembezoni mwa barabara. Wakati kila mmoja akitaka kuangalia wapi sauti ile ilikuwa inatoka, tayari aliyefanya kitendo hicho alikuwa ameingia kwenye gari lilioondoka kwa kasi ya mshale.

Gari nyeupe aina ya Toyota Alphard iliondoka na kukata kulia kwenye barabara inayoelekea Goba ili kuwepa foleni. Umati wa watu ulianza kukusanyika eneo ambalo mtoto huyo alinyakuliwa. Kama kawaida ya wakazi wa Dar es salaam, walifurika eneo lilipofanyika tukio kila mmoja akijifanya mhadithiaji mzuri na ameliona tukio hilo vizuri zaidi kuliko mwenzake.

Ukweli unabaki pale pale kuwa ni tukio lililofanyika ndani ya sekunde kadhaa, zisizodidi 40 tu. Ilionekana jamaa aliyefanya kitendo hicho na aliyekuwa ndani ya gari walikuwa wazoefu au walilifanyia mazoezi tukio hilo.

Ilikuwa ni saa tisa alasiri wakati watoto wanakwenda kupanda basi la shule lililokuwa limepaki nje ya geti la shule, hiyo iliyopo maeneo ya Mbezi, pembeni tu mwa barabara ya Bagamoyo.

“Yaani mwanangu ilikuwa kama muvi ya kimafia hivi, jamaa kama taa, kamnyakua dogo nini, gari ilikuwa umepaki pale mlango ulikuwa wazi, yaani ili kupiga hatua nne tu kaingia naye kwenye gari, dereva akapiga msele huo, mlango ulifungwa wakati gari linaondoka.” Mmoja wa vijana aliyedai kuona tukio hilo kwa usahihi zaidi aliwaambia watu.

“Ukiambiwa uende kutoa ushahidi utakubali?” Mwenzake mmoja akamuuliza. “Aaah! Hayo sasa mengine, nani aende kutoa ushahidi.” Akajibu na kusababisha umati kuangua kicheko.

Dakika 15 baadaye ikathibitisha kuwa mwanafunzi Macaire Macky, ndiye aliyetekwa. Ni mwanafunzi mdogo tu mwenye umri wa miaka sita anayesoma darasa la kwanza katika shule hiyo. Awali ilithibitishwa na baadhi ya wanafunzi wenzake.

Baadaye walimu nao walikuja eneo la tukio na kuthibitishwa na wanafunzi wao kuwa mwenzao mmoja amemnyakuliwa na mtu ambaye hawamfahamu.

**“Niambie mwalimu nini kimetokea?” “Bwana Macky pole sana na hii ni pole ya wote. Muda wa jioni ambao wanafunzi wanatoka, mtoto wetu, yaani Macky, ametekwa.” “Ametekwa?” Macaire akauliza kwa mashangao kana kwanza ndiyo kwanza anaipata hiyo taarifa.**

******************************

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Tom Academy, Dickson Kisanga alitazama saa kwenye mkono wake wa kushoto kwa mara ya tatu sasa. Ilikuwa ni kila baadaye dakika 15 hivi alifanya hivyo. Alitegemea wageni wawili ofisini mwake. nao ni wazazi wa mwanafunzi wake Macky aliyetekwa. Baada ya tukio lile hakuondoka ofisini kama ilivyo kawaida. Mlio wa bodaboda uliiishia karibu na ofisi yake. Akategemea mgeni au wageni wowote muda ule.

Mlango wa ofisi uligongwa. Halafu ukasukumwa kama ulivyoandikwa kwa mtu yoyote aliyetaka kuingia.

Aliyeingia alikuwa ni mwanaume kijana aliyekomaa, aliyeonekana kufikia umri wa miaka 30 hivi. Aliingia akiwa ametahayari lakini akijaribu kuficha kile kilichokuwa moyoni mwake. “Karibu.” Mwalimu akamkaribisha.

Akamuonyesha sehemu ya kukaa. Haikuwa mara ya kwanza kwa watu hao wawili kuonana. Mara nyingi walionana kukiwa na matatizo kwa mtoto Macky, au mikutano ya shule.

“Niambie mwalimu nini kimetokea?” “Bwana Macky pole sana na hii ni pole ya wote. Muda wa jioni ambao wanafunzi wanatoka, mtoto wetu, yaani Macky, ametekwa.” “Ametekwa?” Macaire akauliza kwa mashangao kana kwanza ndiyo kwanza anaipata hiyo taarifa.

“Ndiyo, ila tumesharipoti haraka polisi na walifika eneo la tukio na kufanya uchunguzi wa awali, ikiwa ni pamoja na kuchukua maelezo ya wanafunzi wenzake jinsi mwenzao alivyochukuliwa. Hata wafanyabiashara na baadhi ya abiria waliokuwa kituoni, wachache walioona walichukuliwa maelezo yao pale pale na kesho tutakwenda kwenye kituo cha polisi cha kati kusikiliza kile ambacho watatuambia walipofika, au kutupa maelekezo nini cha kufanya.” Maneno yaliyoonekana ya kisiasa au ya kumpoza hayakumridhisha Macky, akaamua kumuuliza mwalimu. “Hivi hawa watekaji wanatafuta nini? Kumteka mtoto mdogo kama yule? Ana kosa gani mwanangu? Maana kama ni mkubwa unaweza kusema aligombana na watu fulani, au kuchukuliana wanawake, sasa huyu mtoto mdogo, malaika aliyejua chochote.” Maneno ya uchungu yalimtoka baba wa watu. Mwalimu Kisanga kwanza alimuacha baba Macaire aongee na kutoa uchungu wake, maana uchungu wa mwana aujuae mzazi. Baadaye akainuka na kumfuata pale alipo kitini. Akampiga mgongoni. “Macky, wewe ni mwanaume. Unatakiwa kutulia na kusubiri uchunguzi wa Jeshi la Polisi ili kubaini ni watu gani wamehusika na hili na sababu ni nini. Nadhani hawatoshindwa kitu. Wana raslimali zote zinazoweza kuwafanya wahisika wakamatwe. Ila tu sisi huku inabidi tuombe Mwenyezi Mungu ili mtoto apatikane akiwa hai, kwani mpaka sasa ni kweli hakutujui dhamira halisi ya watekaji.” Wakati akaambiwa hayo, Macky alikuwa amejiinamia, machozi kwa mbali yalionekana kumtoka, ingawa alionekana kujizuia sana kuonekana analia.

“Najua kuwa mkeo mlitengena muda mrefu, ndiyo maana kwenye mikutano unakuja wewe, mama yake anakuja mara chache sana, kwa maana hiyo nimempigia pia mzazi mwenzako naye nadhani anaweza kuwasili mida hii hii, maana kaniambia anakuja, inawezekana foleni tu imemchelewesha.” “Ni kweli, kuna foleni sana, mimi mwenyewe niliamua kushuka kwenye daladala na kuchukua bodaboda ili nifike haraka.” Macky aliongea kwa unyonge. “Vipi unamsubiri?” Mwalimu akauliza. “Hapana hata nguvu ya kumsubiri mtu hapa sina. Halafu unajua watoto wa kike, akakuja analia hapa halafu tuanze kazi ya kubembeleza tena badala ya kufikiri nini kitafanyika. Tena imekuwa vizuri sana mimi nimekuja kabla yake.” Akasema Macky huku akinyanyuka.

“Basi Mwalimu kesho tutakutana kituo cha polisi mjini.” “Tuombe Mungu.”

Walitoka nje ya ofisi na kwa sababu hapakuwa mbali sana na barabara, mwalimu alimpeleka hadi kituoni, huku akimpa maneno ya faraja kuwa hakuna baya lolote litakalomfika mtoto.

“Nashukuru, tuendelee kuomba Mungu, ila mwalimu simu yangu ipo wazi hata usiku wa manane, lolote litakalotokea utanipigia.” “Haina neno, we nenda kampumzike.”

Baada ya kuhakikisha amepata usafiri, mwalimu Kisanga akarejea ofisini kwake haraka kwani alitegemea kupata ugeni mwingine wa mama mzazi wa Macaire baada ya baba yake kuondoka. Na kweli alipofika nje ya ofisi yake alimuona mwanamke ambaye alionekana analia akiwa ameshikiliwa na mwanaume mwingine. Wala haikuhitaji kuuliza kama yule ndiye mama Macaire.

*Itaendelea Jumapili*



## ALI KIBA HATAKI UTANI NA MTU

MSANII nguli wa muziki wa bongo fleva nchini, Ali Kiba ameachia albamu au EP yenye ngoma saba akiwa amewashirikisha baadhi ya wasanii wengine wakubwa nchini.

Kiba ameipa jina la 'Starter', EP hiyo ambayo ngoma zake zimeshaanza kuwagusa mashabiki wa muziki huyo.

Ngoma zilizopo kwenye albamu hiyo ni, 'Nahodha', 'Top Notch akimshirikisha Marioo, kuna pini nyingine inaitwa 'Kheri', kuna nyingine inaitwa 'Hatari', ambayo humo wamemuweka Jay Melody, 'Bilando' ambayo ndani kuna sauti na mwanadada, Nandy, 'Chibaba', na 'Nahodha', 'Nahodha Acoustic.'



# P DIDDY HANA PA KUCHOMEKEA

MWANAMUZIKI wa muziki wa hip-hop duniani P Diddy, amenyimwa dhamana kwa mara nyingine tena baada mabishano makali wa mawakili wa pande zote mbili.

Mwanamuziki huyo ambaye jina lake kamili ni Sean John Combs, yupo rumande akisubiri hatma ya kesi yake ya biashara ya ngono inayomkabili.

Baada ya mabishano, hatimaye Jaji wa shirikisho mjini New York alimuweka rumande mwanamuziki huyo baada ya waendesha mashtaka kudai kuwa kama angepewa dhamana kuna hatari mshtakiwa huyo angetoroka.

Bwana Combs, mwenye umri wa miaka 54, alikamatwa wiki hii, akishutumiwa kwa kuendesha biashara ya uhalifu kuanzia mwaka 2008 iliyohusisha dawa za kulevya, unyanyasaji wa kuwalazimisha wanawake, ili kutimiza tamaa zake za ngono, kwa mujibu wa waendesha mashtaka.

Pia P Diddy, ana mashtaka mengine ya ulaghai, biashara ya ngono, na usafiririshaji haramu wa watu ili kwa ajili ya kutumikisha ukahaba.

Mwenyewe amekana mashtaka yote na iwapo atapatikana na hatia ya makosa yote matatu, rapa huyo na mtayarishaji rekodi anakabiliwa na kifungo cha miaka 15, au kifungo cha maisha jela.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GREENWOOD AGOMBEWA
BARCELONA, Atletico Madrid na Bayern Munich ni miongoni mwa klabu zinaomhitaji mshambuliaji wa Marseille, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22. ***(Talksport)***

### PSG INAMTAKA ISAK
KLABU ya PSG inamtaka mshambuliaji wa Newcastle United raia wa Sweden, Alexander Isak huku Magpies hao wakiweka thamani ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kuwa takriban euro milioni 100. ***(Fichajes)***

### DISASI KUUZWA JANUARI
CHELSEA inataka kumuuza mlinzi wa Ufaransa, Axel Disasi mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Fichajes)***

### YILMAZ ATAKIWA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest inawafuatilia wachezaji wawili wa kimataifa wa Uturuki, winga wa Galatasaray, Baris Alper Yilmaz mwenye umri wa miaka 24 na mshambuliaji wa Besiktas, Semih Kilicsoy mwenye miaka 19. ***(HITC)***

### TONEY ALITAKIWA ARSENAL
ARSENAL ilikutana na mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28, kipindi cha majira ya joto, badala yake alikwenda kwa klabu ya Saudi Arabia ya Al-Ahli. ***(TBR Football)***

### JUVE INAMTAKA DAVID
JUVENTUS inataka kumsajili mshambuliaji wa Lille na Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24 Januari kwa mkataba wa euro milioni 15. ***(Calciomercato)***


### GASIOROWSKI ATAKIWA MADRID
REAL Madrid inafikiria kufikia kiwango cha euro milioni 45 ambacho ni kipengele cha lazima katika suala la kumnunua beki wa Valencia mwenye umri wa miaka 19 raia wa Hispania, Yarek Gasiorowski. ***(AS)***

### EVERTON YAMUWANIA CALVERT
KLABU ya Everton itampa mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin fursa ya mwisho ya kusaini mkataba mpya kabla ya mkataba wake kumalizika msimu ujao wa joto, huku Newcastle United ikionesha nia ya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Teamtalk)***

### WALKER-PETERS HAKIELEWEKI
MAZUNGUMZO mkataba mpya kati ya Southampton na mlinzi wa England, Kyle Walker-Peters yamegonga mwamba huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye miaka 27 ukikamilika msimu ujao wa joto. ***(Fabrizio Romano)***

### EUSTACE AJUMUISHWA
KLABU ya Southampton imemjumuisha kocha wa Blackburn, John Eustace kwenye orodha yao huku ~~watakatifu hao wakifikiria nani wa kuchukua nafasi~~ ya Russell Martin. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
# MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI: WACHEZAJI WATAKATWA MISHAHARA

●●●NI wale watakaocheza mechi chache kutokana na kuchoshwa na kalenda mpya na...

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema anaamini wachezaji watakuwa tayari kupunguzwa mishahara ikiwa itamaanisha kucheza mechi chache zaidi msimu huu.

Wachezaji bora wa kimataifa wanaoshiriki michuano iliyopanuliwa ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la klabu bingwa ya Dunia lililoboreshwa wanaweza kucheza mechi 85 msimu huu, jambo ambalo limesababisha baadhi ya wachezaji kulalamika kuhu- [redacted]

sababu lengo ni kujaribu kucheza mechi chache ili kuwa na majeraha kidogo," alisema Ancelotti alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Iwapo hiyo itasababisha kupunguzwa kwa mishahara, lengo ni wachezaji kucheza michezo michache kwa hiyo sidhani kama wachezaji watakuwa na shida ya kupunguza mishahara yao ikiwa watacheza mechi chache."

Mapema wiki hii, kiungo wa kati wa Manchester City, Rodri alionya kwamba wachezaji wako karibu kugoma kwa sababu ya wasiwasi [redacted]

Wachezaji kadhaa, akiwemo Thibaut Courtois wa Real Madrid na Dani Carvajal wamemuunga mkono Rodri.

Ancelotti alisema tishio la wachezaji hao kugoma halitabadilisha kalenda ya msimu huu.

"Malalamiko ya makocha na wachezaji hayatabadilisha kalenda ya msimu huu," alisema Ancelotti.

"Ni muhimu kutafakari juu ya hili na wachezaji zaidi kwa sababu wanachoka. Inabidi tulichambue hili. Wachezaji wanafikiria kuhusu mabadiliko katika siku zijazo."

# FERGUSON: NAIMISI SANA KUINOA MAN

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson amekiri kuwa bado anamisi maisha ya ukocha katika dimba la Old Trafford.

Ferguson alijijengea heshima kama mmoja wa makocha wakubwa wa wakati wote katika kipindi cha miaka 27 ndani ya United ambayo ilitoa mataji 13 ya Ligi Kuu ya England na mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kuondoka kwenye wadhifa huo na kustaafu mwaka 2013.

Akiwa bado anahusishwa na klabu nyuma ya pazia, Ferguson amekiri kwamba bado anafikiria kuhusu wakati wake kama kocha.

"Ninaimis wakati mwingine," alisema Ferguson akiimbia BBC Breakfast.

"Mwaka wa kwanza baada ya kustaafu nilikwenda fainali ya Ulaya na nikamwambia mkewe wangu marehemu Cathy: 'Hiki ndicho ninachokikosa, michezo mikubwa, michezo ya Ulaya'.

"Hivyo basi niliend a kwenye fainali nyingi za Ulaya kwa sababu nilipata kitu ndani yake ambacho ninaweza kuhusiana nacho, kitu ambacho ningependa kufanya kila siku. Kwa sababu haya ni matukio makubwa ambayo klabu kama United inapaswa kuhusika kila wakati."

United wanaendelea kujitahidi kurejea katika viwango vya juu chini ya Ferguson.

David Moyes, Louis van Gaal, Jose Mourinho, Ole Gunnar Solskjaer na sasa Erik ten Hag wote wamechukua mikoba tangu kustaafu kwake miaka 11 iliyopita.




# Alexander-Arnold kununua timu Ufaransa

**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold anatazamiwa kuwa mmiliki mpya wa klabu ya FC Nantes inayoshiriki Ligi kuu ya Ufaransa, Ligue 1, katika hatua ambayo imeshitua wadau wa soka duniani.

Beki huyo wa kimataifa wa England amekuwa akihusishwa na kuondoka Anfield msimu ujao baada ya mkataba wake kumalizika.

Kumekuwa na uvumi wa kitasa hicho cha Arne Slot kuhamia kwa miamba ya LaLiga, Real Madrid kwa uhamisho wa bure lakini inaonekana kama Alexander-Arnold anaweza kuwa na timu yake binafsi hivi karibuni.



Gazeti la Ufaransa L'Equipe linadai kwamba Alexander-Arnold yuko tayari kutoa ofa ya euro milioni 100 ili kuwa mmiliki wa FC Nantes ya nchini Ufaransa kupitia mfuko mmoja wa uwekezaji wa nchini England unaosimamiwa na baba yake mzazi.

Gazeti hilo linadai Kylian Mbappe 'anawahamasisha' wanasoka wengine kuchukua hatua katika umiliki wa klabu baada ya mshambuliaji huyo wa Real Madrid hivi majuzi kununua asilimia 80 ya hisa za klabu ya Ligue 2 nchini humo Stade Malherbe Caen.

Mfanyabiashara Mfaransa, Waldemar Kita, ambaye amekuwa akimiliki Nantes tangu 2007, inaonekana amechoshwa na matatizo ya kimichezo na kifedha yanayokabili eneo la pwani ya magharibi mwa Ufaransa la Loire-Atlantique.

# Van Dijk hataki Liverpool kupoteza nyumbani

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk amedhamiria kwamba Liverpool isiwe na 'tabia' ya kupoteza michezo nyumbani.

Wekundu hao walipata kichapo cha kushangaza cha 1-0 nyumbani kwa Nottingham Forest baada ya mapumziko ya kimataifa ya Septemba, na hivyo kuhitimisha mwanzo mzuri wa maisha wa kocha Arne Slot hapo Merseyside.

Hii ilifuatiwa na ushindi wa kishindo wa 3-1 dhidi ya AC Milan katika Ligi ya Mabingwa Ulaya katikati ya wiki.

Nahodha wa klabu hiyo, Van Dijk amejivunia rekodi ya juu zaidi Anfield tangu kuwasili kwake katikati ya msimu wa 2017/18, na katika maelezo yake, aliwataka wachezaji wenzake kuhakikisha nyumba yao inabaki ngome imara.

"Tunajua kwamba tulipungukiwa na kiwango kinachohitajika dhidi ya Forest, na hiyo inaumiza," alisema Van Dijk.

"Hatupotezi mechi nyingi kwenye uwanja wa Anfield, kwa hiyo ilikuwa lazima kwamba watu walikuwa wanashangaa jinsi tungefanya tulipokuwa tukielekea Milan. Na mbali na dakika tano za kwanza, nadhani tulijibu maswali.

"Kama nilivyosema hapo awali, hatupotezi mechi nyingi Anfield, na hiyo sio tabia tunayotaka kuanza sasa.

"Tulionesha hisia nzuri pale Milan, na sasa tunataka kuwapa mashabiki wetu kitu cha kupiga kelele baada ya kukatishwa tamaa wikendi iliyopita."



## HABARI MICHEZO

# TANZANIA YATAMBA KUFANYA VIZURI KUFUZU MASHINDANO YA KRIKETI

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA wa timu ya taifa ya Kriketi, Muthumudalige Pushpakumara, amesema wamejipanga kuhakikisha wanapata nafasi moja wapo kati ya mbili za kufuzu kwenda kusaka tiketi ya kucheza michuano ya dunia ya mchezo wa Kriketi.

Tanzania ni mwenyeji wa michuano ya wanaume ya kufuzu mashindano hayo ya dunia kutoka nchi za Afrika ambayo yameanza jana jijini Dar es Salaam na kushirikisha nchi sita za Cameroon, Ghana, Lesotho, Malawi, Mali na wenyeji.

Akizungumza na Nipashe jana, Pushpakumara alisema amekiandaa vizuri kikosi chake kwa ajili ya kushindana na kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mashindano hayo yanayofanyika jijini Dar es Salaam.

“Nimewandaa vizuri wachezaji wangu, nataka wawe frii kucheza lakini wacheze kwa malengo, tunawachezaji ambao wamecheza pamoja kwa muda mrefu na wamezoeana hii inanipa matumaini ya kufanya vizuri ukiangalia na namna tulivyojiandaa,” alisema Pushpakumara.

alisema kikubwa anataka wachezaji wake wafurahie kucheza mashindano hayo na kuonyesha uwezowake kwa kuwa wana uwezo wa kufanya hivyo.



Kocha wa timu ya taifa ya mchezo wa Kriketi, Muthumudalige Pushpakumara (kushoto) akiwa na nahodha wa timu hiyo, Abhik Patwa, wakizungumzia jana maandalizi ya timu hiyo kuelekea mashindano ya kufuzu fainali za Dunia za ICC yanayofanyika Jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

Nahodha wa timu ya hiyo, Abhik Patwa,alisema wachezaji wote wapo katika hali nzuri tayari kuanza mashindano hayo na wana hofu na timu yoyote.

“Hatuangalii viwango vya timu nyingine kwenye orodha ya timu bora, kikubwa ni maandalizi mazuri na wao wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanafikia malengo yao,” alisema Patwa.

Alisema kwa sasa mchezo wwa kriketi unazidi kukuwa Afrika na anaamini ni zamu ya Tanzania sasa kufanya vizuri na kufuzu kwa fainali hizo za dunia kama zilivyobaadhi ya nchi za jirani ambazo zimewahi kufuzu fainali hizo.



Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao (katikati), akiwa na viongozi na wageni waalikwa wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Kigoma (KFA), uliofanyika kwenye hoteli ya Lake Tanganyika juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Azam, Coastal wapaniana

***

**Na Shufaa Lyimo**

USHINDI ni kauli ya makocha wa pande zote kuelekea kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara leo kati ya Azam FC dhidi ya Coastal Union, utakaochezwa majira ya saa 1:00 usiku kwenye uwanja wa Azam Complex.

Azam itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu nzuri ya kuichapa timu ya KMC mabao 4-0 katika mchezo wao uliopita ambao ulichezwa Septemba 19 mwaka huu kwenye uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Akizungumzia mchezo huo jana, Kocha Mkuu wa timu ya Azam, Rachid Taoussi alisema wamejipanga vema kuhakikisha wanapata pointi tatu katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa.

“Kila mchezaji ana morali ya juu kuelekea kwenye mchezo huo kwa maelekezo na mbinu nilizowapa wachezaji wangu naamini tutapata pointi tatu katika uwanja wetu wa nyumbani,”alisema Taoussi.

Kwa upande wake Lusajo Mwaikenda ambaye alizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake alisema wamejipanga vema kuhakikisha wanaendeleza ushindani waliouonesha walipokutana na KMC.

Alisema licha ya kuwa Coastal Union ina wachezaji wazuri watafuata maelekezo waliyopewa na benchi lao la ufundi ili wapate matokeo mazuri.

Kwa upande wake Kaimu Kocha Mkuu wa Coastal Union, Joseph Lazaro alisema amewaandaa vizuri wachezaji wake ili wapate ushindi japo anafahamu wanakutana na timu nzuri.

# Simba kazi moja tu leo

INATOKA UK. 24

Kidemokrasi ya Congo anayesemekana kuwa yupo nchini kwa ajili ya kumalizana na klabu ya Simba ili kujiunga kipindi cha dirisha dogo la usajili, atakuwepo jukwaani akiiangalia timu ambayo ilikuwa ajiunge nayo kipindi cha usajili mkubwa uliopita, lakini akapata ofa ya kwenda nchini Ubelgiji kufanya majaribio yaliyofeli katika klabu ya Klabu ya Genk.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema mchezo wa leo utakuwa tofauti na ule wa mwanzo waliocheza ugenini.

Alisema katika mchezo wa mwanzo, awali aliingia kuzuia na kushambulia kwa kushtukiza ili kusaka bao, lakini baada ya kuona wapinzani wao wanaingiza washambuliaji wengine, hasa kipindi cha pili, ndipo akaamua kupaki basi ili kuzuia wasipate bao.

“Hii ni tofauti na hapa, tutakachofanya ni kuzuia, lakini tutakwenda mbele kusaka mabao. Hatutaki wapinzani wetu waanze kupata bao kabla ya sisi kwa sababu utatuweka kwenye wakati mgumu na presha kubwa, tunachotaka ni kuwa na ukuta mgumu usiofungika, halafu ndiyo tunatafuta bao, tukilipata najua wataondoka nyuma kwa ajili ya kusaka bao la kusawazisha, hapo ndipo tutakapopata mwanya wa nafasi nyingi zaidi,” alisema Fadlu raia wa Afrika Kusini.

Mechi ya leo imekuwa na presha kuwa hasa kwa wapinzani ambao wamekodisha mabaunsa wa kuwalinda wakihofia kulipiziwa kisasi kwa kile ambacho mashabiki wao walikifanya Jumapili iliyopita.

Mashabiki wa Al Ahli Tripoli, waliwafanyia fujo wachezaji na baadhi ya viongozi wa Simba, kabla, wakati wa mchezo na baada, kitu ambacho kiliifanya klabu hiyo kushtaki kwenye Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Hata hivyo, Rais wa CAF naye akiwa nchini Nairobi nchini Kenya, aliagiza uchunguzi ufanywe na hatua zichukuliwe kwa kile kilichotokea kwenye mchezo huo.

Kama itatinga makundi itakuwa ni mara ya pili kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, kama ilivyofanya msimu wa 2021/22 na kufanikiwa kufika hatua ya robo fainali.



Michezo
Jumapili Septemba 22, 2024
Nipashe



## Ancelotti: Wachezaji watakatwa mishahara

UKURASA 21

## Gamondi aiona Yanga ikishinda ubingwa Afrika

**Na Faustine Feliciane, ZANZIBAR**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amesema anaiona Yanga ikiwa karibu na kutwaa ubingwa wa Afrika kwa miaka ya karibuni kutokana na viwango vya wachezaji na uongozi mzuri walionao kwa sasa.

Akizungumza jana kabla ya mchezo wao wa marudiano wa hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE ya Ethiopia, Gamondi, amesema kwa sasa Yanga ni moja ya timu kubwa na ya kuogopwa Afrika kutokana na uwezo wao.

"Kwa namna timu inavyoendeshwa na usajili unaofanyika kila dirisha la usajili linapofika naiona Yanga ikifanikiwa zaidi kwa miaka ya karibuni, ni timu yenye malengo, hii inatokana na aina ya uongozi walionao," alisema Gamondi.

Alisema mafanikio waliyoyapata katika misimu ya karibuni ni kielelezo tosha cha namna ya mwelekeo mzuri wa timu hiyo katika kufikia mafanikio waliyoyakusudia.

"Msimu uliopita tulikuwa na malengo ya kucheza hatua ya makundi, tulifanikiwa na kufikampaka robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini nyuma yake timu hii iliceza fainali ya Kombe la Shirikisho, hapo utaona ni timu inayopanda juu kwenye mafanikio ya Afrika," alisema Gamondi.

Gamondi akuacha kuizungumzia Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo amesema ni ya ushindani na yenye msisimko mkubwa miongoni mwa Ligi za Afrika.

"Ligi hii inavutia wachezaji wengi kuja kucheza hapa, hii inatokana na ushindani wake na msisimko uliopo, mashabiki wake ni watu wanaoongeza chachu kwenye ligi, ndio maana unaona timu za Tanzania zinfanya vizuri zaidi ukilinganisha na timu nyingine za Afrika Mashariki kwenye mashindano ya CAF," alisema Gamondi.

Mara baada ya mchezo wa jana usiku uliochezwa uwanja wa New Amaan Stadium, Yanga sasa inarejea kwenye michezo yake ya Ligi Kuu ambapo jumatatu inategemea kusafiri kuelekea Mbeya kwa ajili ya mikikimikiki ya Ligi hiyo.



Wachezaji wa Simba wakiongozwa na Kibu Dennis wakati wa mazoezi ya kujiandaa na mchezo wa leo wa Kombe la Shirikisho Afrika, CAF, dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA KAZI MOJA TU LEO

## ●●●Yasaka tiketi kutinga makundi CAF, Mpanzu jukwaani...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika michuano ya Kombe la Washindi Afrika, Simba, leo saa 10:00 jioni watashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, wakiwa na dhamira moja tu ya kuhakikisha wanatinga hatua ya makundi dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya.

Maxi Nzengeli

Simba inatarajia kukamilisha mipango yake hiyo leo baada ya Jumapili iliyopita kulazimisha suluhu ugenini dhidi ya timu hiyo iliyokuwa nyumbani, Uwanja wa Juni 11, jijini Tripoli.

Ni ushindi wowote ule ndiyo utaivusha Simba kwenye hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Mechi hiyo inayotarajiwa kuhudhiriwa na maelfu ya wanachama na mashabiki wa Simba, itashuhudiwa pia na mchezaji wa zamani wa AS Vita, Elie Mpanzu ambaye yupo nchini.

Winga huyo raia wa Jamhuri ya

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >